SUPA JACKPOT
TZS. 1,027,393,141
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.co.tz
PIGA *150*87#



UKURASA 3

## RC Makalla atoa msimamo stendi binafsi za mabasi


Tukidekezana kwa mambo ya msingi hatutafika

BUFE

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

Nipashe

KUSUASUA KIWANDA CHA CHAI MPONDE..
Ziara ya Komredi Chongolo yawasha moto ghafla yapata uhai, waziri na RC watinga

Asimulia TASAF ilivyowafanyia maisha yaeleweke kwa plau cherehani, baiskeli

UKURASA 11

Ijumaa Septemba 2, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581056

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

# Kilio wananchi tozo chasikika

## WATAALAMU kukuna vichwa upya...

*Endelea ukurasa wa 2*



Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, akitoa ufafanuzi kuhusu tozo kwenye miamala ya simu na benki katika mkutano na waandishi wa habari jijini Dodoma jana. Kushoto ni Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge na Uratibu, George Simbachawene. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Viwanja vidogo marufuku hati

UKURASA 2



UKURASA WA 7

## BOT, TPA, WIZARA ELIMU ZABANWA HOJA ZA CAG

KAMATI ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) imeiagiza Benki Kuu ya Tanzania (BoT) kujibu hoja zote za ukaguzi kabla ya ukaguzi mpya kuanza huku Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) akiagizwa kuhakiki majibu ya hoja hizo ili zifungwe...

UKURASA WA 7

## VIGOGO WA HALMASHAURI WATIMULIWA BUNGENI

KAMATI ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) imeirudisha Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo kutokana na kutotekeleza maagizo 30 ya kamati hiyo. Akitoa maazimio ya kamati hiyo juzi baada...

UKURASA WA 7

## JELA MIAKA 70 KUNAJISI MTOTO

MAHAKAMA ya Wilaya ya Bariadi mkoani Simiyu imemhukumu Kulwa Meleka, mkazi wa Bariadi, kutumikia kifungo cha miaka 70 gerezani na kulipa faini ya Sh. milioni moja kwa makosa ya kumtorosha mtoto wa kike mwenye umri wa miaka 13 na kisha kumnajisi.



UKURASA WA 19

## KESI PINGAMIZI URAIS KENYA YAPAMBA MOTO

MAHAKAMA ya Juu nchini Kenya imeelezea kuwa mchakato wa kuingia kwenye mfumo wa mtandao wa teknolojia wa Tume ya Uchaguzi na Mipaka (IEBC) umekamilika.

Kwa mujibu wa taarifa iliyochapishwa jana na DW, Jaji Isaac Lenaola wa jopo la majaji saba aliielezea Mahakama ya Juu kuwa walipokea ripoti kamili ya kikosi cha ufundi...

# Waziri afunguka magumu ya NHIF

UKURASA 3



Mfanyakazi wa basi la Shabiby, Lucas Jeremiah, akimkatia tiketi abiria kwa njia ya mtandao katika Stendi Kuu ya Mabasi ya Magufuli, Mbezi Luis mkoani Dar es Salaam jana. **Habari Uk. 3. PICHA: MIRAJI MSALA**

MICHEZO YANGA: KISINDA ATATUBEBA CAF UK.24 KABWELA UK. 18

# Viwanja vidogo marufuku hati

**Na Romana Mallya**

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angelina Mabula, amesema uwiano wa moja kwa moja wa kiwanja cha 20/20 haukubaliki, kwa sababu hakuna viwanja vyenye upana na urefu wa namna hiyo, hivyo havitapata hati za umiliki.

Aidha, ameagiza kampuni binafsi za upangaji, upimaji na nyingine zinazojihusisha na masuala ya ardhi na yeyote anayejihusisha na uuzaji wa vipande vya ardhi kwa mtindo huo, kusitisha kazi hizo na kurejesha fedha kwa wananchi kwa maeneo ambayo tayari kuna migogoro.

Waziri Mabula aliyasema hayo jana mkoani Dar es Salaam wakati akifungua mkutano wa siku mbili wa wadau wa uendelezaji milki.

Alisema kwa mujibu wa sheria ya Mipango Miji Na. 8 ya mwaka 2007, Sura 355, kifungu 77 (1) (b), (i), Kanuni ya Viwango vya Upimaji Maeneo, zilizotangazwa kwenye gazeti la serikali namba 91 na 93 la Machi 9, 2018, ukubwa wa maeneo kwa matumizi mbalimbali umeainishwa.

"Kwa mujibu wa sheria hii na taaluma ya mipango miji, viwanja vya matumizi mbalimbali vinatakiwa kuwa na ujazo tofauti, ujazo wa juu, ujazo wa kati na ujazo wa chini. Viwanja hivi vinatakiwa kuwa na mapana na marefu yenye uwiano wa moja kwa mbili mpaka moja na mbili na nusu.

"Kwa mfano, kiwanja chenye ukubwa wa mita za mraba 400 kinapaswa kuwa katika uwiano wa upana wa mita 16 na urefu 25. Uwiano wa moja kwa moja 20/20 haukubaliki kitaaluma na hakuna kiwanja chenye upana na urefu ulio sawa," alisema huku akibainisha kuwa taaluma ya mipango miji inaelekeza mpangilio wa viwanja kuhusiana na ujazo.

Waziri Mabula aliagiza bodi zote za kitaalam kuanzia Bodi ya Usajili Wataalam wa Mipango Miji, Baraza la Wapima Ardhi Tanzania na Bodi ya Usajili ya Wathamini, kufanya uchunguzi wa kampuni zote zinazofanya kazi kinyume na sheria ili hatua kali zichukuliwe haraka. "Nitoe rai kwa wananchi, kuwa makini na watu wanaowauzia ardhi kwa aina hii, kabla ya kununua ardhi mwananchi hakikisha unapata taarifa au mwongozo kutoka ofisi za ardhi ziliko halmashauri au ardhi mkoa ili kupata ushauri," alishauri.

Kiongozi huyo alisema hivi karibuni kutokana na thamani ya ardhi kupanda kumekuwapo na idadi kubwa ya makazi na uwepo wa kampuni binafsi upangaji na upimaji ardhi.

"Kumetokea wimbi kubwa la uuzaji holela wa viwanja ambavyo havizingatii matakwa ya sheria ya mipango miji, kwa baadhi ya kampuni na wakala wa ardhi wamekuwa wakigawa na kuuza viwanja ambavyo havijapangwa wala kupimwa kwa jina maarufu 20/20.

"Hili ninalizungumzia kwa sababu viwanja ni fursa ya kujitafutia kipato, katika suala la kupanga viwanja 20/20, na wanakwenda maeneo ambayo pengine Halmashauri haijapima, wanawakatia watu na kuwauzia," alisema.

Alisema wanahitaji watu wapate viwanja ambavyo wanaweza kuzalisha shughuli za kiuchumi na siyo vya tamaa za fedha za haraka haraka.

"Kama wizara tumepiga marufuku, sitaki kuona wala kusikia, mpima yeyote atakayepitisha kiwanja cha aina hii 300, 400, 500, yaani katika upimaji wako huna ujazo wa juu, ujazo wa kati na ujazo wa chini kwenye maeneo yako?" aliwahoji.

Waziri Mabula alisema hivi karibuni wizara imekuwa ikipokea maombi kutoka kwa wananchi wakitaka kupimiwa maeneo yao, ambayo wanadai wameshauziwa lakini eneo halijapangwa wala kupimwa. Alibainisha kuwa kampuni hizo zimekuwa zikinunua maeneo na kukata viwanja vidogo vidogo vyenye ukubwa wa mita za mraba 300 bila kuzingatia sheria na mahitaji ya huduma za jamii kisha kuwauzia wananchi.

"Ukiangalia hakuna maeneo ya barabara na yaliyotengwa hayafiki hata mita nne kwenye eneo hilo, baada ya kuwauzia wananchi wanawaelekeza waende kwenye wizara kwa ajili ya kupimiwa. Wakati huo huo wameshauza na kuleta migogoro. "Kampuni hizi tumeshazibaini na tutaangalia namna ya kuzichukulia hatua, nielekeze bodi zinazohusika kuanza kuwabaini mmoja baada ya mwingine kwa sababu wengine tunao kwenye mitandao, hili ni jambo ambalo haliakisi taaluma yako."

Waziri huyo alisema kampuni inapima ili ijipatie faida lakini anayepimiwa anaingia kwenye matatizo na mengine yanapimwa yakiwa na milki tayari.

Alimtaka mkurugenzi wa sekta milki kwa kushirikiana na bodi zinazohusika (mipango miji na wapima), kuhakikisha watu wa namna hiyo wanashughulikiwa.

Pia aliwaonya wale wote wanaopitisha ramani (Wapima wa Mikoa) katika wizara kwa kuwaeleza kuwa hategemei siku tano mbele baada ya agizo hilo wapitishe ramani kinyume.

Waziri Mabula alisema bado sekta ya milki ina changamoto, ikiwamo uhaba mkubwa wa nyumba hususani zenye bora na zile za gharama nafuu ambapo nchi ina upungufu wa takribani nyumba milioni 3 na ongezeko la mahitaji ya wastani nyumba 200,000 kwa kila mwaka.

Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Dk. Allan Kijazi, alisema serikali inafanya maboresho makubwa ya sera na sheria katika milki na kwamba watakuwa wakikutana mara kwa mara ili kuibua changamoto na mikakati mipya.



Rais Samia Suluhu Hassan, akimpa pole Rais mstaafu wa Awamu ya Pili, Ali Hassan Mwinyi, kufuatia kifo cha mtoto wake Hassan Ali Mwinyi, baada ya kuwasili nyumbani kwa marehemu Chukwani, mjini Zanzibar jana, kwa ajili ya kuhani msiba. Wa pili kulia ni Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi. **PICHA: IKULU**

# Kilio cha wananchi tozo chasikika

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imesema imesikia kilio cha wananchi kuhusu tozo za miamala ya simu na benki pamoja na kodi ya upangishaji majengo na kwamba inafanyia kazi hoja zilizotolewa na wananchi kuhusu mambo hayo na hivi karibuni itatoa tamko la utekelezaji wake.

Pia imesisitiza kuwa uamuzi wa kuweka tozo hizo ulifanyika kwa kushauriana na wananchi.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa jana, Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, alisema baada ya kuibuka malalamiko, wamekutana na makundi mbalimbali kushauriana ikiwamo Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi na wataalamu wa kodi na maoni yao yalilenga kutozwa tozo mara mbili.

"Serikali imesikia wananchi wametoa maoni ya msingi na nia yao ni kujenga. Tumepokea na tunafanyia kazi na tutatoa majibu kwenye utekelezaji wake siku si nyingi. Tutatoa utaratibu, kuweni watulivu wakati tunashughulikia," alisema.

"Serikali imejiridhisha kuwa baadhi ya taasisi za fedha zilianza kukusanya tozo husika tarehe 15 badala ya Julai Mosi. Tutakutana na taasisi za fedha tutakaa, nchi hii ni yetu wala mtu asipate hofu kutoa maoni," alisema.

Kuhusu malalamiko ya kodi ya upangishaji wa majengo, Dk. Nchemba alisema kodi hiyo si ya mpangaji na kwamba hawajibiki na hana mapato yanayotokana na kupangishwa nyumba bali mwenye nyumba.

"Serikali tumepokea tunafanyia kazi suala la kugeuka kuwa mkusanya kodi. Tutatoa tamko tunapokwenda kwenye utaratibu kulingana na maoni ya wananchi," alisema.

Dk. Nchemba alisema kuna timu inaendelea kuchambua mifumo ya kodi ili kuwa na wigo zaidi ikiwamo kuangalia Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT).

"Tozo hii si faida ya biashara bali chimbuko lake ni ushirikiano wa pamoja wa kuunganisha nguvu kutekeleza majukumu haya ni ya lazima ambayo yamekuwa yakikosa fedha kibajeti," alisisitiza.

Alisema kama taifa kuna majukumu ya msingi ambayo kila Mtanzania anatakiwa kuyabeba huku akibainisha kuwa: "Mwanzo tulivyoanza wananchi walisema tumeenda kwa kiwango kikubwa bali tupunguze halafu tuongeze wigo."

Dk. Mwigulu alisema tozo hizo zilizoanzishwa kwenye bajeti ya mwaka 2021/22, zimekuwa msaada mkubwa kwa taifa kwa sababu zimesaidia kuchochea maendeleo kupitia miradi mbalimbali inayotekelezwa hapa nchini.

"Ni tozo. Ndiyo ina maumivu ya hapa na pale na tunatambua kweli kwamba inavuruga 'purchasing power' ya mtu mmoja mmoja lakini tuna majukumu ambayo kama nchi na sisi wote kama wazazi tunawajibika kuyabeba kama wajibu wetu," alisema.

Waziri huyo alisisitiza mapato ya tozo katika mwaka wa fedha 2021/22 ni Sh. bilioni 221 zilighharimia mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu na Sh. bilioni 117 zilitumika kujenga vituo vya afya.

Alisisitiza kuwa tozo hizo zimeendelea mwaka huu (2022/23) kwa sababu kuna majukumu ya msingi ambayo serikali haiwezi kuyaahirisha.

"Hapa tulipo hatuwezi kuahirisha bwawa la Nyerere, hatuwezi kuahirisha reli ya kisasa. Tuliona tusiahirishe shughuli za uzalishaji na matunda yake mtayaona baadaye," alisema.

Mwaka huu, alisema serikali imepanga kujenga madarasa yasiyopungua 8,000 ili wanafunzi watakaojiunga na kidato cha kwanza mwaka 2023 wakae vizuri kwenye madarasa.

Pia alisema serikali kwa mwaka huu imeweka nguvu kubwa kwenye shughuli za uzalishaji kutokana na tatizo la ajira kwa vijana ikiwamo zaidi ya Sh. bilioni 900 kupelekwa Wizara ya Kilimo.

"Kila wanapomaliza darasa la saba kuna watoto 200,000 hawajiungi na kidato cha kwanza na wanapomaliza kidato cha nne watoto 300,000 hawaendelei kidato cha tano. Watu 500,000 hadi milioni moja hawaingii kwenye mfumo mmoja wa elimu, tumewahi kujiuliza wanakwenda wapi? 'Equation' ya nchi yetu imebadilika sana, umri wa nchi yetu ni wa nguvu kazi," alisema.

"Nawashukuru Watanzania nilifuatilia utafiti wa Twaweza wakasema wanaunga mkono tozo na wengine walisema tukielekezwa inafanya nini watatunga mkono, sasa tuna majukumu haya ambayo hayaepukiki," aliongeza.

Awali, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Bunge, George Simbachawene, alimtaka Dk. Mwigulu kuwa na jukwaa maalumu kwa ajili ya kutoa ufafanuzi juu ya mambo yanayojadiliwa mtandaoni.

Naye Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Innocent Bashungwa, alisema vituo vya afya 234 vimejengwa kutokana na fedha za tozo ya miamala ya simu ndani ya mwaka mmoja tangu kuanzishwa kwake.

"Kupitia tozo za miamala ya simu, tumeweza kujenga vituo vya afya 234 kwa Sh. bilioni 117 kwenye tarafa 207 na kila kituo cha afya kimetugharimu Sh. milioni 500," alisema.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu,Kazi,Ajira,Vijana na Watu Wenye Ulemavu, Prof. Joyce Ndalichako, aliwatoa wasiwasi wafanyakazi kuwa walikaa na viongozi wao wa vyama vya wafanyakazi kujadiliana kuhusu hilo na serikali imepokea mawazo yao na inafanyia kazi.

# Tiketi mtandao zaanza na dosari

**Na Waandishi Wetu**

LICHA ya serikali kuagiza wamiliki wa mabasi yaendayo mikoani na nchi jirani kutumia tiketi za kielektroniki kuanzia jana, utekelezaji wa agizo hilo ni kitendawili.

Nipashe jana ilifika Stendi Kuu ya Magufuli ya Mabasi Yaendayo Mikoani na kujionea baadhi ya mawakala wakikatisha tiketi za karatasi badala ya kutoa kwa mfumo wa kielektroniki.

Mfumo wa tiketi za kielektroniki ulianza kufanyiwa majaribio Aprili Mosi mwaka huu na jana ilikuwa ni siku rasmi ya kuanza kutumika.

Mmoja wa mawakala wa ukataji tiketi katika stendi hiyo (jina limehifadhiwa), alisema mfumo wa tiketi mtandao umeanza na unaendelea lakini tiketi za mkononi zinatolewa.

Alisema mfumo wa tiketi za kielektroniki una tatizo la kimtandao, kwamba wakati mwingine unasumbua na kusababisha msongamano wa abiria wanaohitaji huduma.

Wakati kadhia hiyo ikitokea, Meneja Mradi wa Tiketi Mtandao kutoka Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA), Tadei Mwita, alisema tiketi za mkononi zinapatikana kwa sababu baadhi ya kampuni na abiria walichelewa kujiunga na mfumo wa tiketi mtandao.

"Mwitikio juu ya tiketi mtandao umepokewa vizuri na abiria pamoja na wasafirishaji japo kuna tatizo la kimtandao hasa wale waliochelewa kujiunga na mfumo lakini tunalifanyia kazi ili kulitatua," alisema Mwita.

Mwakilishi wa Mabasi ya Kampuni ya Simba Mtoto, Mohamed Ibrahim, alisema: "Mchakato ni mzuri kwani tiketi za mkononi zina ubabaishaji na tatizo la kimtandao ni dogo sana, sisi tunaunga mkono mchakato huu na abiria wetu wamelipokea vizuri."

Mwakilishi wa Kampuni ya Golden, Josia Adam, alisema wameupokea vyema mfumo mpya wa tiketi mtandao na abiria nao wameupokea.

Nipashe ilizungumza na baadhi ya abiria katika stendi hiyo akiwamo Maika Mapunda ambaye aliipongeza serikali kwa kuanzisha mfumo wa tiketi mtandao unaorahisisha kupata tiketi kwa wakati bila usumbufu.

Aliwaomba wamiliki wa mabasi kuwa na mashine zaidi ya moja ili kuondoa msongamano wa abiria ndani ya stendi.

Abiria mwingine, Mohamed Ally, alisema: "Sikupata tatizo lolote kwani mfumo wa tiketi mtandao ni mzuri na nimetumia dakika mbili kupata tiketi yangu."

Mkoani Mwanza jana kulitokea shida katika matumizi ya mfumo huo, baadhi ya abiria walitaka tiketi mtandao wakiachwa katika Stendi Kuu ya Mabasi ya Nyegezi.

Mmoja wa abiria hao, Athumani Omary, alisema: "Nilikata tiketi yangu saa mbili usiku, lakini hadi muda huu sijapata gari la kupanda, nikimpigia wakala aliyenikatia tiketi hii hapatikani, nimejaribu kuuliza askari wa usalama barabarani akanieleza kuwa endelea kusubiri gari labda litakuja."

Mkurugenzi wa LATRA, Johansen Kahatano, alishuhudia hali hiyo alipozuru katika stendi hiyo na kuwakuta abiria wakiendelea kusubiri bila mafanikio.

"Hili ni tatizo, lakini tunafanya utaratibu wa kuona namna ya kuwapatia usafiri mbadala abiria hawa ili kuendelea na safari zao, lakini niwaeleze kuwa kwa sasa serikali imeweka mkakati wa ukataji wa tiketi kwa njia ya kielektroniki ambayo inasaidia kupunguza matatizo ya kiuhalifu kama haya yanayofanywa na mawakala wasio waaminifu," alisema.

■**Imeandaliwa na Victoria Mgodomi, Owen Bariki, Joram Gervas (TUDARCo), Evence Evarist (DSJ), Vitus Audax (MWANZA).**




Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, akizungumza na waandishi wa habari jijini Dodoma jana, kuhusu mwenendo wa huduma za Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), zitakavyotolewa na mapungufu yaliyojitokeza hadi kusababisha kuyumba kwa mfuko. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Waziri afunguka magumu ya NHIF

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Afya, Ummy Mwalimu, amesema kukosekana kwa uaminifu kwa wanachama na watu wanaojiunga wakiwa wagonjwa ni miongoni mwa sababu za kuelemewa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF).

Katika kuzingatia hali hiyo, Ummy ametaja mikakati mbalimbali ya serikali kuunusuru mfuko huo usife ikiwamo kuja na muswada wa bima ya afya ya lazima kwa watu wote ambao upo hatua za mwisho kuwasilishwa bungeni.

Akitoa jana ufafanuzi kwa umma kuhusu mfuko huo kuwa kwenye hatari ya kufilisika, Waziri Ummy alisema tatizo la NHIF lilianza baada ya kuruhusu kuingiza wanachama wa hiari ikiwamo Toto Afya Kadi ambapo asilimia 99 wanaojiunga na NHIF kwa hiari ni wagonjwa.

"Kuna mwingine mtoto yupo hospitalini anatakiwa kufanyiwa upasuaji, labda siku hizi tumeona kuna kuibuka watoto wanaozaliwa bila njia za haja kubwa, tutakuja kutoa taarifa tumeona ongezeko, gharama yake ni Sh. milioni 1.2, NHIF ukikata kadi kwa Sh. 50,400 baada ya mwezi mmoja inaanza kutumika.

"Mtu amechangia Sh. 50,400 anakwenda kupata huduma ya Sh. 600,000 ndani ya mwezi mmoja. Idadi ya watoto waliojiandikisha kwenye Toto Afya Kadi ni 180,000.

"Sasa tunakuja na suluhisho, kama tutasema bima ya afya ni hiari, watajiunga hawa wagonjwa, tuna zaidi ya watoto milioni 20, ikiwa bima lazima NHIF akisajili watoto milioni tano tu watahudumia watoto wagonjwa," alisema.

Waziri Ummy alisema mkakati uliopo ni kuongeza wanachama wa NHIF ambao wanaamini watakuwa siyo wagonjwa.

"Serikali ipo hatua za mwisho kuja na sheria ya bima ya afya kwa wote ambapo tunaamini ikiwa ni lazima, tutakuwa na idadi kubwa ya Watanzania ambao siyo wagonjwa wawachangie wachache walio wagonjwa. Kuna mtu analipia kifurushi Sh. 600,000 kila mwezi, anafanya vipimo na dawa," alisema.

Waziri huyo alibainisha kuwa hadi sasa NHIF ina wanachama milioni 4.8 kati ya Watanzania zaidi ya milioni 60 wakati mwaka 2011/12 ilikuwa na wanachama 691,000.

"Idadi ndogo ya wanachama ndiyo inaweka hatari ya mfuko kuwa kwenye hatari ya uhai wake. Suluhisho ni kuja na sheria itakayokuwa na bima ya afya lazima," alisema.

**UDANGANYIFU**

Waziri Ummy pia alisema watumishi kwa sasa wameibuka mtindo wa kuwaondoa watoto kwenye utegemezi na kuweka wazazi wagonjwa.

"Anamtoa mtoto wake kwa sababu haumwi, anamwingiza baba mkwe mgonjwa. Sasa kwanini NHIF isiwe kwenye hatari? Nimeelekeza NHIF kuliangalia hili maana mtu anaingizwa na magonjwa yasiyo ya kuambukiza ambayo yana gharama kubwa za matibabu," alisema.

Pia alisema kuna udanganyifu wa baadhi ya watoa huduma za afya na kusisitiza hawatavumilia mtoa huduma atakayebainika kufanya hivyo.

"Asilimia 70 ya mapato ya hospitali yanategemea mapato ya NHIF, suluhisho lake nimewataka NHIF waimarishe mifumo ya uthibiti kwa kutumia TEHAMA ndani ya siku 14 waniletee mpango wa utekelezaji wake.

"Kuna maduka ya dawa yalikuwa yanatumika mtu anarundikiwa dawa 10, hilo tunalifanyia kazi, lazima wazingatie miongozo ya serikali ya matibabu," alisema.

Mkurugenzi Mkuu wa NHIF, Bernard Konga, alisema mwaka 2021/22, vituo 29 vilibainika kuwa na udanyanyifu wa Sh. bilioni 7.9 na kusitisha mikataba.

# RC Makalla atoa msimamo wa stendi binafsi za mabasi

**Na Mary Geofrey**

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla, ametoa msimamo kuhusu stendi za mabasi binafsi na kuondoa katazo la mabasi yaendayo mikoani na nje ya nchi kutoruhusiwa kupakia abiria au kushusha katika vituo hivyo isipokuwa kituo kikuu cha Magufuli, Mbezi, Dar es Salaam.

Kwa agizo hilo, ametangaza kurejeshwa utaratibu wa awali wa kuendelea kushusha abiria kwenye vituo binafsi vya abiria kwa sharti la kila basi kuingia ndani ya Kituo Kikuu cha Magufuli kabla ya kwenda kwenye vituo binafsi. Makalla alitangaza uamuzi huo jana Dar es Salaam wakati wa kikao cha pamoja baina ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri wa Ardhini (LATRA), wamiliki wa stendi binafsi na Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo.

Kupitia kikao hicho walijiridhisha pasipokuwa na shaka kuwa wamiliki wa mabasi waliokuwa wakishusha abiria kwenye vituo vyao walifuata taratibu na kupatiwa vibali na LATRA baada ya kukidhi vigezo. Miongoni mwa vigezo vilivyotolewa na LATRA ili kuruhusiwa kuanzisha stendi binafsi ni pamoja na uwapo wa vyoo, sehemu ya mapumziko kwa abiria, viburudisho na sehemu za maegesho. Kutokana na hilo, Makalla aliridhia vituo binafsi vitano vilivyohakikiwa kuendelea kutoa huduma na kufungua milango kwa wamiliki wengine wanaohitaji kuwa na vituo binafsi, kushirikiana na LATRA ili kupatiwa vigezo vinavyohitajika na wamepewa mamlaka ya kufuta au kutoa leseni.

Aidha, Makalla aliagiza Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo kukaa kikao mara moja na wamiliki wa stendi binafsi ili kuona njia bora ya ukusanyaji wa mapato. Jana, Nipashe liliripoti habari ya wananchi wakilalamikia utaratibu wa mabasi kushusha abiria kwenye kituo Kikuu cha Mabasi cha Magufuli peke yake kuwa ni usumbufu kwa abiria wanaoishi jirani na vituo binafsi vya mabasi.

Juzi, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Innocent Bashungwa, alimwagiza Makalla kukaa meza moja na wadau na wamiliki wa mabasi hayo ili kuweka utaratibu mzuri wa namna ya mabasi hayo kuingia kituo cha Magufuli.

# Wakazi Wazo waomba punguzo fidia saruji

**Na Waandishi Wetu**

WAKAZI wa Tegeta Kata ya Wazo maeneo ya Chasimba, Chatembo na Chachui, Kinondoni mkoani Dar es Salaam, wameiomba serikali kuangalia uwezekano wa kupunguza gharama za fidia wanayodaiwa na Kiwanda cha Saruji cha Wazo Hill.

Ombi la wananchi hao limekuja siku moja tangu Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla, kuwataka wananchi hao kulipa fidia ndani ya mwezi mmoja au kuhama eneo hilo mali ya kiwanda hicho.

Wakizungumza jana na Nipashe kwa nyakati tofauti, wananchi hao waliomba kupunguziwa gharama hizo kulingana na hali duni ya kipato chao kwa kuwa wanategemea biashara ndogondogo kuendesha familia.

"Muda tuliopewa ni mdogo na pesa ni nyingi kwa sababu kipato chetu ni kidogo halafu unaambiwa lipa Sh. milioni mbili na nyumba zenyewe tunazoishi tunashindwa kuzitengenezea mazingira mazuri. Je, hiyo fedha ya kulipa tutatoa wapi?" alihoji Kulthum Ibrahim.

"Ni muhimu wakaangalia mazingira tunayoishi si watutajie gharama ambazo hatuzimudu. Wanavyosema ndani ya mwezi mmoja tuhame inakuwa si haki kwetu kwa sababu tumekaa muda mrefu na serikali inatambua," alisema Mussa Ismail.

Pia walisema kuwa kuna mabadiliko juu ya gharama za upimaji katika maeneo huku wakidai upimaji huo ni tofauti na awali na kwamba kila mkazi mwenye kiwanja alitakiwa kulipa Sh. 1,000 kwa mita moja ya mraba na nyaraka zipo lakini hivi sasa wametakiwa kulipa Sh. 6,400 kwa ukubwa huo.

Meneja wa Mazingira katika Kiwanda cha Saruji Wazo, Richard Magoda, alikanusha kuwapo makubaliano ya awali na wananchi hao kwa ajili ya kupima kiwanja kwa gharama ya Sh.1,000 kwa mita moja ya mraba.

"Nyaraka ni karatasi sio maneno kwahiyo hakuna kiwanja kinachouzwa Sh.1,000 mita moja ya mraba wanatakiwa kulipa Sh.6,400 kwa mita moja ya mraba," alisema.

Juzi, RC Makalla aliongeza mwezi mmoja kwa wananchi hao kuhama au kulipa fidia ili waendelee kuishi na kwamba kuna viongozi watapita nyumba kwa nyumba kutoa ankra ya malipo na kila mmoja atatakiwa kutia saini na kama hawataki watachukuliwa hatua.

**Imeandikwa na Aisha Kondo, Saumu Hassan na Said Muhibu**




Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Selemani Jafo (kulia), akijadiliana jambo na Balozi wa Uingereza nchini, David Concar, wakati wa ufunguzi wa Mkutano wa Mabadiliko ya Tabianchi na Maendeleo jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Jela miaka mitano kuua mtoto wa mkewe

**Na Joctan Ngelly,** GEITA

MAHAKAMA Kuu Tanzania Kanda ya Mwanza iliyoketi Geita, imemhukumu mkazi wa Busambilo Wilaya ya Bukombe, Anthony Masai (40), kutumikia kifungo cha miaka mitano jela kwa kosa la kumuua mtoto wa mke wake.

Mtoto huyo mwenye umri wa miezi saba, Elizabeth Stephen, aliuawa kwa kutupwa chini na kichwa kikabonyea hatimaye kufariki dunia.

Hukumu hiyo ilitolewa jana na Hakimu Mkazi Mfawidhi Mkoa wa Geita aliyepewa mamlaka ya ziada Cleofas Waane, baada ya mshtakiwa kukiri kumuua bila kukusudia mtoto huyo.

Baada ya kukiri kosa, Hakimu Mkazi Waane alimwambia Wakili wa Serikali Winfrida Ernest, amsomee mshtakiwa maelezo ya awali.

Akimsomea maelezo ya awali, Wakili Ernest alidai kuwa mshtakiwa alikuwa akiishi na mke wake, Tabu Mwanga, katika kijiji cha Busambilo na aliolewa akiwa na watoto akiwamo Elizabeth ambaye alikuwa mtoto wa kambo.

Ernest alidai kuwa Agosti 9, 2017 mshtakiwa alikuwa na mke wake kilabuni wakiwa wanakunywa pombe hadi majira ya saa 6:00 usiku na kuanza siku mpya ya Agosti 10 na baadaye Tabu aliitwa na mwanamume mwingine na kuondoka naye akimwacha mshtakiwa kilabuni.

Alidai kuwa mshtakiwa aliporudi nyumbani, hakumkuta mke wake na punde kidogo mke alirudi na mshtakiwa alimuuliza ulikuwa wapi. Baada ya hapo ugomvi ulitokea na kuanza kupigana na mke wake baada ya kuona amezidiwa, alikimbia na kumwacha mtoto akiwa amelala hapo kitandani kisha mshtakiwa alimchukua mtoto huyo na kumpiga chini, kichwa chake kikabonyea na kufariki dunia papo hapo.

Pia alidai kuwa baada ya mshtakiwa huyo kuona mtoto halii, alimchukua pamoja na wanazengo na kumpeleka katika kituo cha afya Ikonya na walipofika, walielezwa kuwa mtoto ameshafariki dunia.

Alidai kuwa daktari aliyefanya uchunguzi wa mtoto huyo, alibaini kuwa alifariki dunia kwa sababu ya damu kuvilia kwenye ubongo baada ya kutupwa chini hadi kichwa kikabonyea.

Ernest alidai kuwa mshtakiwa alikamatwa na kupelekwa Kituo cha Polisi Bukombe na baada ya mahojiano, alipelekwa mahakamani ili sheria ichukue mkondo wake.

Baada ya Wakili wa Serikali kumaliza kumsomea mshtakiwa maelezo ya awali, Hakimu Mkazi Waane alimuuliza kama yote yaliyosomwa ni kweli au si kweli, ndipo akajibu ni kweli tupu.

Hakimu Waane alisema: Mshtakiwa kwa kuwa umekiri kosa lako mwenyewe bila kulazimishwa, mahakama hii inakutia hatiani kwa kosa la kumuua mtoto Elizabeth Stephen.

Pia mahakama hii inakutaka ujitetee ili kukupunguzia adhabu."

Wakili wa Kujitegemea Penina Mashimba, alidai kuwa mteja wake amekaa gerezani miaka mitano na amejifunza ndiyo maana amekiri kosa lake na pia hajaisumbua mahakama na kuokoa gharama za mahakama, hivyo mahakama impatie adhabu ndogo hasa kifungo cha nje.

Upande wa Jamhuri ukiongozwa na Wakili Ernest, aliomba mahakama itoe adhabu kali kwa kuwa kitendo alichokitenda ni cha kinyama cha kulipisha kisasi mtoto wa miezi saba ambaye hana kosa lolote na wala hakuhusika katika ugomvi wao.

Hakimu alitupilia mbali utetezi huo na kusema mshtakiwa kitendo ulichokifanya ni cha kinyama. Hivyo mahakama inakuhukumu kifungo cha miaka mitano jela ili akajifunze huku akitaka upande ambao haujaridhika unaweza kukata rufani.

# Nape: 5G itaipaisha Tanzania kiuchumi

**Na Halfani Chusi**

MTANDAO wa 5G uliozinduliwa jana na Kampuni ya Mawasiliano ya Simu ya Vodacom Tanzania, umetajwa kuwa na faida zitakazoisaidia nchi kupanua wigo wa biashara na kurahisisha mambo mbalimbali katika sekta ya mawasiliano.

Mkoani Dar es Salaam jana, Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye, wakati wa uzinduzi wa mtandao huo alibainisha kuwa mfumo huo utaleta mapinduzi makubwa ya kidijitali na kuipeleka Tanzania katika ramani ya dunia.

Alisema Vodacom wanastahili pongezi kwa kuiweka Tanzania kuwa miongoni mwa nchi chache katika Bara la Afrika zinazotumia mtandao wa 5G, akifafanua kuwa hali hiyo inadhihirisha umahiri wao katika sekta ya mawasiliano.

"Kama mnavyofahamu, serikali imedhamiria kujenga mazingira rafiki kwa maendeleo ya teknolojia ya mawasiliano nchini. Hii ni kutokana na dhana kwamba maendeleo katika TEHAMA (Teknolojia ya Habari na Mawasiliano) yanachangia kwa kiasi kikubwa kutatua matatizo mbalimbali katika jamii.

Vodacom wamekuwa mstari wa mbele kwa kuleta huduma bunifu kwa kutumia uwezo wao wa kiteknolojia, mfano huduma walizozindua hivi karibuni ikiwamo ya (M-MAMA) inayookoa maisha ya wanawake na watoto, (M-MKULIMA) inayokwenda kuleta mageuzi katika sekta ya kilimo pamoja na (M-PESA) ambayo imeleta mageuzi makubwa katika masuala ya kifedha.

"Ninaomba na kampuni zingine ziige mfumo huu kama una uwezo wa kusaidia mtu ambaye hayupo hapa na ukamwona na kuongea naye kama yupo, hii ni teknolojia kubwa sana, lakini pia kuna faida nyingi sana kupitia huu mtandao wa 5G sekta nyingine zitanufaika kama nishati, madini, ujenzi wa viwanda, kilimo, afya, elimu na usafiri," alisema.

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, alisema mtandao huo utarahisisha ufundishaji kwa walimu akidai utamwezesha mwalimu kutoka mkoa mwingine kufundisha mwanafunzi wa mkoa mwingine. "Kama kipindi cha corona shule zilifunga na walimu walishindwa kuendelea na majukumu yao. Kama mfumo huu, ungekuwapo, wanafunzi wangeendelea kupata elimu. "Lakini inawapa wanafunzi namna nzuri ya kujisomea kwa sababu ukiingia mtandaoni unataka kusoma kitu fulani, hutumii muda mrefu kukifungua kwa sababu mtandao huu una nguvu kubwa sana tofauti na 4G. Kwa hiyo hii ni fursa nzuri na ina faida kubwa sana kwetu hasa kwenye mambo ya elimu," alisifu.

Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla, alipongeza kampuni hiyo kwa kubuni na kuleta huduma hiyo, akibainisha kuwa mfumo huo utasaidia katika masuala ya kudumisha ulinzi na usalama.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji Vodacom Tanzania, Hilda Bujiku, alisema mtandao huo umeongezwa ubora na nguvu ambayo itamrahisishia mtumiaji kukichukua kitu kirahisi kutoka mtandaoni tofauti na ilivyokuwa awali.

"Kwa sekunde tatu unaweza ukamaliza kuchukua video mtandaoni tofauti na awali unatumia zaidi ya saa mbili. Kwa hiyo, ninaomba watu wachangamkie fursa kuanzia leo (jana) wateja wanaweza kufika maduka ya Vodacom kwa ajili ya kupata ufafanuzi na kuanza kunufaika na huduma hii," alisema.

## TANGAZO

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA NISHATI

MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI (EWURA)

ewura
Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji
ISO 9001:2015 Certified

# MWITO WA KUTOA MAONI

***Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), ni taasisi ya udhibiti wa huduma za sekta nne mchanganyiko inayojitegemea, iliyoundwa kwa Sheria ya EWURA Sura ya 414 ya Sheria za Tanzania. Shughuli kuu za Mamlaka ni pamoja na kudhibiti kiufundi na kiuchumi sekta za Nishati na Maji kwa Tanzania Bara. EWURA ina wajibu wa kudhibiti shughuli za mkondo wa kati na mkondo wa chini wa sekta ndogo ya Mafuta na Gesi Asili.***

Sheria ya Mafuta Na. 21 ya mwaka 2015 inaipa nguvu EWURA, kusimamia shughuli za mkondo wa kati na mkondo wa chini wa sekta ya mafuta ya petroli. Kifungu cha 131 (1) cha sheria hiyo kinawataka wote wanaojihusisha na sekta tajwa kuwa na leseni iliyotolewa na EWURA.

Kutokana na kifungu cha 19(4) cha Sheria ya EWURA, Sura ya 414 ya Sheria za Tanzania, taarifa inatolewa kwa umma kwamba, wafuatao wameomba leseni kujihusisha na mkondo wa chini wa sekta ya mafuta ya petroli.

| S/N | Jina la Mwombaji | Eneo | Jina la Mkurugenzi/Uraia | Aina ya Leseni/ Kibali |
|---|---|---|---|---|
| 1. | GM and Company (T) Limited, S.L.P. 7788, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 112, Serengeti Reli, Mtwara Mikindani, Mtwara. | Gabriel Michael Kessy Mtanzania) | Leseni ya ghala la Kuhifadhi Mafuta |
| 2. | Centurion Global Limited, S.L.P 71748, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 30, Eneo la Mikocheni, Kinondoni, Dar es Salaam. | Stella Remi Sakia (Mtanzania) | Leseni ya Jumla ya mafuta |
| 3. | Tanoil Investment Limited, S.L.P 2274, Dar es Salaam. | Kiwanja No.10, Kitalu "A', TPDC Undali Flats, Kinondoni, Dar es Salaam Region. | Kapuulya Angetile Musomba (Mtanzania) | Leseni ya Uwakala wa Condensate |
| 4. | China State Farms Agribusiness (Group) Corporation (Tanzania), S.L.P. 123, Kilosa. | Kiwanja Na. 508, Eneo la Rudewa, Kilosa, Morogoro. | Qiu Bin (Raia wa China) | Leseni ya kituo cha mafuta kwa matumizi binafsi |
| 5. | Crescent Energy Tanzania Limited S.L.P. 68121, Pwani. | Kiwanja Na.5, Kitalu "N" Eneo la Chamakweza, Chalinze, Pwani. | Rehema Mwaula (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 6. | Mohamood Mohamed Duale Transporter Ltd, S.L.P. 3260, Dar es Salaam. | Kiwanja Na.64, Kitalu "42" Kinondoni, Dar es Salaam | Mohamood Mohamed Duale (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 7. | Patrick John Sharishoy, S.L.P. 1867, Dar es Salaam. | Eneo la Makangarawe, Temeke, Dar es Salaam. | Patrick John Sharishoy (Mtanzania) | Leseni ya Usambazaji wa gesi ya kupikia (LPG) |
| 8. | Chrive Petroleum – Ngyekye Filling Station, S.L.P 168, Kyela. | Kijiji cha Ngyekye, Mababu, Kyela, Mbeya | Veronica C. Mbunda (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 9. | Vincent Fire Mwamakimbula, S.L.P 102, Kyela. | Kijiji cha Tenende, Kyela, Mbeya | Vincent Fire Mwamakimbula (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 10. | Vincent Fire Mwamakimbula – Pampalano Oil, S.L.P 102, Kyela. | Kijiji cha Mwela, Busokelo, Mbeya | Vincent Fire Mwamakimbula (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 11. | East Africa Crude Oil Pipeline (EACOP) Limited, Msasani Peninsula, 429 Mahando Street, Block D, S.L.P 385568, DAR ES SALAAM. | Mkuza wenye urefu wa kilomita1147 na upana wa mita 30 kuanzia kijiji cha Mtukula wilayani Misenyi mkoa wa Kagera hadi Chongoleani katika mkoa wa Tanga. | Martin Tiffen (Muingereza) | Kibali cha ujenzi wa bomba la mafuta. |
| 12. | Olympic Petroleum Arusha-Njiro, S.L.P 16484, Dar es Salaam. | Kiwanja Na.695, Kitalu "F", Eneo la Njiro, Arusha. | Ally Mohamud Adon (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 13. | Jobu Bosco Fuime T/A Pwaga Petrol Station, S.L.P 200, Mpwapwa. | Eneo la Pwaga, Mpwapwa, Dodoma. | Jobu Bosco Fuime (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 14. | Puma Energy Tanzania Limited, S.L.P. 9043, Dar es Salaam | Eneo la Seronera-Fort Ikoma, Serengeti, Mara. | Dominic Dhana (Mzimbabwe) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 15. | Star Fuel Company Limited, S. L. P. 11223, Dar es Salaam | Kijiji cha Makere, Kasulu, Kigoma. | Ghulamrasoul Abdulrahim Miah (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 16. | NGS Petroleum Limited, S. L. P. 20, Bariadi. | Kiwanja Na. 1, Kitalu 'D', Eneo la Uyovu, Bukombe, Geita. | Njalu Daudi Silanga (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 17. | Quick Services Station Co. Limited, S. L. P. 34, Muleba. | Kiwanja Na. 1176, Kitalu 'B', Eneo la North Buswelu, Ilemela, Mwanza. | Beach Evarist Makaga (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 18. | Nyakato Gas, S. L. P. 55194, Dar es Salaam | Eneo la Buswelu, Ilemela, Mwanza. | Gasper Hosea Laseko (Mtanzania) | Leseni ya Kusambaza Gesi ya Kupikia ya LPG |
| 19. | HOPE Service Station S. L. P. 839, IRINGA | Eneo la Mazimbu, Wilaya ya Morogoro Mjini, Mkoa wa Morogoro. | Mohamed Mansour Huwel (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta kwa matumizi binafsi |

Mtu yeyote au kikundi cha watu wenye pingamizi kwa mwombaji yeyote wa leseni hapo juu kwamba asipewe leseni, anatakiwa kuwasilisha pingamizi hilo kwa EWURA ndani ya siku kumi na nne (14) kuanzia tarehe ya tangazo hili kupitia anwani tajwa hapa chini.

**Imetolewa na**
**Mkurugenzi Mkuu,**
**Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji**

217025702

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Hili la viwanja 20/20 litolewe elimu

**SERIKALI** kupitia Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, imeeleza kutovitambua viwanja vyenye vipimo vya 20/20 na kutaka wote waliopimiwa warudishiwe fedha zao.

Sababu iliyotolewa ni kuwa ukubwa huo haukubaliki kwa sababu hakuna viwanja vyenye upana na urefu wa namna hiyo kisheria.

Pia imeagiza kampuni binafsi za upangaji, upimaji na mengine yanayojihusisha na masuala ya ardhi na kuuza vipande vya ardhi kwa ukumbwa huo, kusitisha.

Serikali imechukua hatua hiyo kwa mujibu wa Sheria ya Mipango Miji Na. 8 ya mwaka 2007, sura 355, kifungu Na. 77 (1) (b), (i), kanuni ya viwango vya upimaji maeneo, zilizotangazwa kwenye Gazeti la Serikali namba 91 na 93, inayoainisha ukubwa wa maeneo kwa matumizi mbalimbali.

Ufafanuzi ni kwamba viwanja hivyo vinatakiwa kuwa na mapana na marefu yenye uwiano wa moja kwa mbili mpaka moja na mbili na nusu.

Mfano uliotolewa ni kiwanja chenye ukubwa wa mita za mraba 400 kinapaswa kuwa katika uwiano wa upana wa mita 16 na urefu 25.

Kutokana na ufafanuzi huo Waziri mwenye dhamana ya ardhi ameagiza bodi zote za kitaalamu kuanzia ya Usajili Wataalamu wa Mipango Miji, Baraza la Wapima Ardhi Tanzania na Bodi ya Usajili ya Wathamini, kufanya uchunguzi wa kampuni zote zinazofanya kazi kinyume na sheria ili hatua kali zichukuliwe haraka.

Kwetu sisi tunasema jambo hili ni jema, lakini swali linakuja kwa wale ambao tayari wameshapimiwa viwanja hivyo kwa makosa na kuweka makazi yao ya kudumu, wanasaidiwa vipi.

Sheria ipo na watu wanaopaswa kuisimamia ili isivunjwe ndiyo wanaopitisha viwanja hivyo mpaka kufikia hatua ya mtu kupewa hati.

Wanaokwenda kupima viwanja hivyo ni watu wenye taaluma ya masuala ya ardhi na wanaelewa ukubwa unaotakiwa kwa viwanja hivyo, lakini wameendelea kuchukua fedha za watu wakijua ni kosa kisheria.

Waliopimiwa na kupata hati za viwanja hivyo pia wamekuwa kwenye orodha ya wanaolipia viwanja vyao kwa mujibu wa sheria inavyotaka na kujiona ni wamiliki halali.

Leo anapoambiwa kuwa viwanja hivyo havitambuliki ni kumweka kwenye njia panda.

Hata hivyo, serikali imewataka wananchi kuwa makini na watu wanaouzia ardhi kwa aina hiyo kabla ya kununua kwa kupata taarifa au mwongozo kutoka ofisi ya ardhi ziliko halmashauri au ardhi mkoa ili kupata ushauri.

Tunavyofahamu wananchi wanaponunua ardhi ni lazima waanzie kwenye ngazi ya serikali ya mtaa kujiridhisha kuwa eneo analouziwa halina tatizo na kisha kwenda ardhi ambako hupata taratibu za kupimiwa mpaka kupata hati.

Kilichoishtua wizara ni kuibuka kwa uuzaji holela wa viwanja ambavyo havizingatii matakwa ya sheria ya mipango miji na baadhi ya kampuni na wakala wa ardhi kugawa na kuuza viwanja ambavyo havijapangwa wala kupimwa maarufu 20/20.

Wananchi wameshauriwa kupata viwanja ambavyo wanaweza kuzalisha shughuli za kiuchumi.


Wizara imesema imekuwa ikipokea maombi kutoka kwa wananchi wakitaka kupimiwa maeneo yao, ambayo wanadai wameshauziwa, lakini eneo halijapangwa wala kupimwa.

Ilibainisha kuwa kampuni zimekuwa zikinunua maeneo na kukata viwanja vidogo vidogo vyenye ukubwa wa mita za mraba 300 bila kuzingatia sheria na mahitaji ya huduma za jamii kisha kuwauzia wananchi.

Viwanja hivyo vinaelezwa kuwa havina huduma za jamii, barabara na wakati huo huo wameuza na kuleta migogoro.

Waziri ameibainisha kuwa kampuni hizo wameshazitambua na kinachoangaliwa ni namna ya kuzichukulia hatua.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Jamani, wakazi Mwanza tunapata tabu kinachojiri stendi mpya Nyamhongolo!

Na Anthony Gervas, MWANZA

**MWEZI** uliopita serikali jijini Mwanza, ilifungua mradi wa stendi kuu mpya ya mabasi yaendayo mikoani 'Nyamhongolo'. Awali hiyo ilikuwa Buzuruga.

Ukweli wa uhalisi wake imezinduliwa, huku ikibaki kuwa na kero mama za vumbi katika kituo kidogo cha daladala, ambacho kipo mahali hapo nyuma ya stendi. Si ajabu mtu kashuka kutoka kwenye basi akiwa na ama kanzu nguo nyingine safi akaoga vumbi kibao!

Ni stendi iliyofunguliwa na kuanza kutumika ikihudumia mabasi yaendayo mikoa ya Mara, Simiyu na wilaya mbalimbali za mkoa Mwanza. Sasa ni jambo linalozua malalamiko ya wananchi wasafiri jijini, kwamba wanapokuwa katika kituo hicho kidogo cha daladala, wanakabiliwa na shida ya vumbi la magari hayo madogo.

Abiria hao wamekuwa wakidai kupata mafua, vikohozi, kuchafuka nguo, majengo ya abiria kujaa vumbi, macho kuuma wakati wakiwa wanasubiria daladala katika kituo hicho, huku eneo lingine ambalo limeunganisha Barabara Kuu ya Nyerere, ambalo halijafanyiwa usafi wa mazingira muda mrefu, limejaa nyasi na halina mtaro wa kupitisha maji.

Pamoja na kufunguliwa stendi hiyo ya kisasa, lakini bado haijakamilika katika eneo hilo na kusababisha kero kwa wananchi wasafiri, wanaohoji kulikoni serikali inafungua mradi ambao haujakamilika kwa ujumla, jambo ambalo inaacha maswali kwa nchi yetu ambayo imeshaingia kwenye uchumi wa kati wa chini.

Iko bayana, watendaji wetu daima hawaishiwi sababu na visingizio katika miradi hiyo mbalimbali kushindwa kukamilika katika kiwango kinachotakiwa.

Ubabaishaji na sarakasi bado zinatawala, huenda na mengime mabaya zaidi ya hayo. Hapo ndipo kunazua msamiati 'mazoea hujenga tabia.' Tuna watendaji wanaofanya kazi kwa mazoea na inawezekana yapo ya kifisadi ndani yake, ambao unapaswa kukatwa, ili kuondoa sababu na visingizio vingi kwa wahusika.

Mimi binafsi naunga mkono hoja za hawa wananchi kuhusu swali lao, kwanini miradi yetu Watanzania huwa haikamiliki katika kiwango kinachotakiwa na kwa wakati? Hivi kuna sababu gani za kufungua mradi mkubwa kama huo wa mabilioni ya shilingi ukiwa haujakamilika ipasavyo?

Ifike mahali sote tuone aibu, nafsi zao ziwakonge wakijua kwamba hiyo miradi Watanzania wote wanapaswa kunufaika nayo na wananchi wanapopaza sauti zao mjue serikali kwamba kuna jambo.

Wananchi wanalalamika kwamba miradi mingi ikiwamo masoko, maeneo waliotengewa Machinga, vituo vidogo vya daladala na stendi za mabasi, kwa asilimia kubwa hujengwa na kufunguliwa bila ya kukamilika ipasavyo, ikiwamo miundombinu kutokuwa rafiki katika kufanya biashara zao.

Jamani Watanzania tunajikwaa wapi? Tuna rasilimali nyingi za kutosha kutekeleza miradi yetu, tuna madini ya kila aina, makaa ya mawe, mafuta, bahari, maziwa matatu yenye samaki wa kila aina, mito, milima na ardhi yenye rutuba ya kutosha.

Katika zama hizi za kuupiga mwingi, ghafla kunapokuwapo watendaji wanaosubiri wasukumwe na wakuu wao na hawawezi kujisimamia wenyewe, ni sawa kweli hawaioni hii adha?

Stendi hiyo iko katika Manispaa ya Ilemela, ambako Mstahiki Meya wake Renatus Mulunga, analipambania hilo kwamba wamepanga bajeti nyingine kuhakikisha vumbi hilo linatoweka mara moja, ili kuondoa adha inayowakabili wasafiri na abiria wanapokuwa wakisubiri magari.

Ninawashauri, wenye uamuzi waondoe fedheha kwa kuwezesha kufunguliwa stendi ninayoitaja ya ambayo sehemu zake zingine hazijakamilika, ujenzi wake hadi sasa bado unaondoa maana ya kuwa na hadhi ya jiji.

Ninashauri serikali ishinikize kukamilishwa mpango wa kukamilisha ujenzi huo haraka kabla ya kipindi cha masika hakijaanza, vinginevyo itaibuka kero nyingine ya kuwepo matope na kuangukia kuwa aibu kwa mradi wote huo.

# Vigogo halmashauri watimuliwa bungeni

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KAMATI ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) imeirudisha Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo kutokana na kutotekeleza maagizo 30 ya kamati hiyo.

Akitoa maazimio ya kamati hiyo juzi baada ya kuhoji Halmashauri za Ngara, Sumbawanga na Biharamulo, Makamu Mwenyekiti wa LAAC, Selemani Zedi, alikumbusha kuwa mara ya mwisho kamati ilipokutana na uongozi wa Halmashauri ya Biharamulo, ilitoa maagizo 33 lakini walipokutana tena juzi, ilibainika wamefanyia kazi maagizo matatu tu.

"Sisi kamati utekelezaji wa maagizo tunauona kama ni utii kwa kamati. Kama walipewa maagizo 33 wakatekeleza matatu, ni asilimia ndogo sana, halmashauri zinazokuja zinakuwa hazijatekeleza yote lakini angalau zimevuka asilimia 50 ya maagizo," alisema.

Kiongozi huyo wa kamati alisema sababu za kutotekelezwa maagizo hayo ni madai kuwa Mkurugenzi wa Halmashauri ni mpya, jambo ambalo kamati haikuona kama ni utetezi wenye mashiko.

"Tumewarudisha ili wakatekeleze maagizo ya nyuma tuliyowapa ili watakapokuja mbele ya kamati, waje wametekeleza. Halmashauri zinapokuja zihakikishe maagizo waliyopewa wameyafanyia kazi ndipo tutoe maelekezo mapya," alisema.

Kuhusu Halmashauri za Sumbawanga na Ngara, Zedi alisema kamati imebaini hazijazingatia upangaji wa makisio ya ndani kutokana na miaka mitatu kuonyesha zimekuwa zikivuka makisio.

"Kamati kwa maoni yetu tumeona halmashuari hizi zinaweza kukusanya mapato zaidi kuliko yaliyowekwa sasa kama wataweza kuzingatia kuweka viwango halisi," alisema.

Aliongeza kuwa kamati imeagiza makisio yao yaendane na uhalisia wa maeneo yao.

"Pia tumebaini utoaji wa asilimia 10 ya mapato ya ndani kwa ajili ya mikopo kwa kinamama, vijana na watu wenye ulemavu wanatenga lakini hawazingatii uwiano wa 4:4:2 kulingana na mwongozo na sheria ya mgawanyo wa fedha hizi," alifafanua.

Zedi alisema ufuatiliaji wa kamati kuhusu urejeshaji wa fedha hizo, umebaini unausua na zinaonekana zipo mikononi mwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

"Pia tumebaini kuna miradi ya maendeleo haijakamilika ya afya na elimu kwenye halmashauri hizo," alisema.

Katika ripoti yake kwa mwaka 2020/22, inayofanyiwa kazi na LAAC kwa sasa, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), pamoja na mambo mengine, amebaini dosari nyingi katika utoaji na urejeshaji wa mikopo itokanayo na asilimia 10 ya mapato ya halmashauri, akishauri serikali ichukue hatua.



Mtaalam wa masuala ya Habari kutoka Taasisi ya Internews Tanzania, Alakok Mayombo (kulia), akizungumza katika ufunguzi wa mafunzo ya masuala ya jinsia kwa waandishi wa habari yaliyoandaliwa na taasisi hiyo, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Jela miaka 70 kunajisi mtoto

**Na Happy Severine,** BARIADI

MAHAKAMA ya Wilaya ya Bariadi mkoani Simiyu imemhukumu Kulwa Meleka, mkazi wa Bariadi, kutumikia kifungo cha miaka 70 gerezani na kulipa faini ya Sh. milioni moja kwa makosa ya kumtorosha mtoto wa kike mwenye umri wa miaka 13 na kisha kumnajisi.

Mtuhumiwa huyo alihukumiwa kifungo hicho juzi wilayani Bariadi baada ya kupatikana na hatia.

Hukumu hiyo ilitolewa na Hakimu Mkazi wa Mahakama hiyo, Caroline Kiliwa, baada ya kutolewa ushahidi na kusikiliza maelezo ya pande mbili.

Kabla ya kutolewa kwa hukumu hiyo, Wakili wa Serikali, Vailet Mshumbushi, alidai mahakamani kuwa mtuhumiwa alitenda makosa hayo kati ya Novemba mwaka jana na Machi mwaka huu katika maeneo tofauti.

Kwa kosa la kwanza la kumtorosha mtoto huyo, Hakimu Caroline alimhukumu mshtakiwa huyo kifungo cha miaka 10 gerezani, kifungo cha miaka 30 kwa kosa la pili la kumpeleka mtoto sehemu isiyojulikana miaka 30 gerezani kwa kosa la tatu la kumnajisi mtoto, faini ya Sh. milioni moja.

Hakimu huyo aliwaonya wale wote wenye tabia kama hizo kuacha mara moja kwa kuwa serikali kupitia vyombo vyake vya usalama haitafumbia macho vitendo vya kinyama.

# BoT, TPA, Wizara Elimu zabanwa bungeni

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KAMATI ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) imeiagiza Benki Kuu ya Tanzania (BoT) kujibu hoja zote za ukaguzi kabla ya ukaguzi mpya kuanza huku Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) akiagizwa kuhakiki majibu ya hoja hizo ili zifungwe.

Makamu Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Japhet Hasunga, akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa juzi baada ya kamati hiyo kuchambua hoja za ukaguzi za CAG kwa mwaka 2020/21, aliagiza hoja hizo zisijirudie katika ukaguzi utakaofanyika wa mwaka 2021/22.

"Tumemtaka CAG aende akahakiki na kuhakikisha hizo hoja zimejibiwa ipasavyo," Hasunga alisema.

Kiongozi huyo wa kamati alikumbusha kuwa BoT katika ukaguzi wa mwaka 2020/21, kuwa kuna hoja 73 na zilizojibiwa ni zaidi ya asilimia 50 na zilishafungwa huku hoja 30 zilibaki pasina kufungwa.

"Kuna hoja zingine zinaihusu BoT lakini ukiangalia zinahitaji mamlaka nyingine ya kwenda kuzifunga. Kwa mfano, iliagizwa baadhi ya fedha zisimamiwe na Benki Kuu lakini sasa hawajapata maelekezo mengine kutoka serikalini hadi Wizara ya Fedha ihakikishe zinafungwa, hizo hoja zinaanzia mwaka 2016 hadi leo," alifafanua.

Kati ya hoja 73 zilizoibuliwa na CAG, ni baadhi ya maofisa waandamizi wa BoT kuziharibu makusudi noti za Sh. 10,000 ili kujipatia mabilioni ya shilingi katika mchakato wa kuchapisha noti mpya.

**SERA YA ELIMU**

Kuhusu fungu la Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Hasunga alisema kamati imeiagiza wizara hiyo iandae mpango kazi wa kuhakikisha wanakuja na sera ya elimu itakayoshirikisha wataalamu na wadau mbalimbali wanaohitajika.

"Tulibaini mambo matatu; cha kwanza ilionekana Sera ya Elimu ya Mwaka 2014 haijatekelezwa vizuri na serikali, pia inakinzana na baadhi ya vifungu vya Sheria ya Elimu ya Mwaka 1978.

"Ilikuwa na msingi mzuri wa elimu, sheria inataka Waziri wa Elimu aunde baraza la wataalamu la kumshauri na baraza hilo halijaundwa. Jambo la tatu lilikuwa kupitia mpango mkakati wa wizara ili kuhakikisha mambo yote ya msingi yanawekwa kwenye hilo," alisema.

Hasunga alisema kuwa baada ya kushauriana, ilionekana ipo haja kwa wizara kupitia upya sera yake ya elimu na kufanya mabadiliko makubwa ya mitaala nchini.

**KIBANO TPA**

Hasunga pia alisema kamati hiyo ilikutana na Mamlaka ya Bandari (TPA) ambapo kwa mwaka huo ilionekana ilipata hati yenye shaka.

"Maeneo manne yaliyosababisha wapate hati yenye shaka ni matumizi ya mfumo wa kufungia hesabu wa COBO. Pili, mifumo mingi waliyokuwa nayo ya kiuhasibu, huo mfumo wa COBO ulikuwa hauonani na mifumo mingine ya kusimamizi wa bandari," alisema.

Hasunga ambaye kitaaluma ni mhasibu mwenye hadhi ya CPA, alisema ilionekana kuna madeni makubwa kwenye vitabu ambayo yalikuwa hayajakusanywa.

"Jambo lingine ni deni la Sh. bilioni 186 lililokuwa linaonekana kwenye vitabu kwamba wanaidai Hazina lakini walikuwa hawajafanya usuluhishi ili kujua kama linaendana. Katika mjadala tumeagiza ufanyike usuluhishi wa hilo deni ili pande zote ziwe na takwimu zinazofanana," alisema.

Hasunga alisema kamati imeagiza waje na mfumo mzuri ambao utakuwa unatumika kuangalia shughuli zote za utendaji za bandari kabla ya kufunga hesabu.

"Kamati imeagiza, hatutaki kuona tena wanapata hati yenye shaka," Hasunga alihitimisha.

# TMDA kuziondoa bidhaa za tumbaku zenye kemikali

**Na Mary Geofrey**

MAMLAKA ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) imesema itaziondoa sokoni bidhaa za tumbaku zinazozalishwa na kuingizwa nchini zenye kemikali sumu, ili kumlinda mtumiaji dhidi ya magonjwa ikiwamo saratani ya damu na koo.

Baadhi ya kemikali sumu 90 zilizopo kwenye tumbaku ni Acetaldehyde, Acetamide, Acetone, Acrolein, Acetamide, Anabasine, Arsenic, Anisidine, O-anisidine, Ammonia, Catechol, Carbon monoxide, Caffeic acid, Cobalt, Furan, Hydrogen cyanide, Lead, Mercury, Nicotine, Nickel, Nitromethane, Ndela, Selenium, Quinoline, Styrene, Uranium 235 na Uranium 238.

Mtendaji Mkuu wa TMDA, Adam Fimbo, alibainisha hayo juzi kwenye maonyesho ya Kimataifa ya Wadau wa Bidhaa za Afya ya Afrika Mashariki maarufu kwa jina la 'Pharmatech East Afrika' yaliyofanyika jijini Dar es Salaam.

"Bidhaa za tumbaku zina kemikali sumu zaidi ya 90 zinazosababisha magonjwa ya saratani. Kwa sasa serikali imewekeza mashine za kisasa za kupimia kemikali sumu katika bidhaa zote za tumbaku ikiwamo sigara na tutapima bidhaa zote za tumbaku ili kulinda afya za watumiaji," alisema Fimbo.

Alisema watafanya ukaguzi kwa bidhaa hizo zote zikiwamo sigara ili kuona kama zina kemikali hizo kabla ya kumfikia mlaji na kusababisha madhara.

"Kemikali sumu zikikosekana kwenye bidhaa za tumbaku zitapunguza magonjwa ya haya na kikubwa hapa tunataka tuwaonyeshe wadau mbalimbali wanaofika kushiriki kwenye maonyesho haya," alisema.

Sambamba na hilo, Fimbo alipiga marufuku uingizaji wa dawa zisizosajiliwa nchini na watakohusika watachukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria ya dawa na vifaa tiba sura ya 219 na adhabu yake ni kuanzia Sh. 50,000 hadi Sh. milioni tano kulingana na kosa.

Alisema kwa sasa dawa zisizosajiliwa zilizopo nchini ni asilimia moja na wanaendelea kutoa elimu kwa jamii kwa njia mbalimbali ili kuwakinga na madhara yatokanayo na matumizi hayo.

Katika maonyesho hayo ya siku tatu yaliyozinduliwa na Naibu Waziri wa Afya, Dk. Godwin Mollel, TMDA inashiriki kutoa elimu kama wadau sekta ya dawa na vifaa tiba kuhusu mambo mbalimbali.



Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki (wa tatu kushoto), na Mwenyekiti wa Kamati ya Kuduma ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, Dk. Christine Ishengoma (wa pili kushoto), wakishuhudia wakati Katibu Mkuu wa Wizara ya Uvuvi, Dk. Rashid Tamatamah (kushoto) na Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB), Frank Nyabundege (kulia), wakionyesha makabrasha jijini Dodoma jana, baada ya kutiliana saini mkataba wa utekelezaji wa mradi wa ununuzi wa boti za uvuvi na vizimba vya kufugia samaki ambao unalenga kuwakopesha wavuvi na wafugaji wa samaki Shilingi Bilioni 32 bila riba. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# GGML yatoa magodoro kwa Kituo cha Wazee

**Na Mwandishi Wetu,** MWANZA

KATIKA kuunga mkono juhudi za serikali kuwajali na kuboresha maisha ya wazee nchini, Kampuni ya Uchimbaji Madini ya Dhahabu Geita (GGML), imetoa msaada wa magodoro 50, kwa Kituo cha Wazee Bukumbi kilichoko mkoani Mwanza.

Akizungumza katika hafla ya kukabidhi msaada huo juzi mkoani Mwanza, Ofisa Mwandamizi wa Uhusiano wa Jamii GGML, Shunashu Musa, alisema msaada huo unalenga kuboresha makazi na hali ya maisha ya wazee wanaoishi katika kituo hicho.

Aliongeza kuwa baadhi ya wafanyakazi wa GGML na wenzao wamekuwa wakisaidia kituo hicho kwa nyakati tofauti na kuchangia baadhi ya vifaa vya matumizi. Kipindi hiki menejimenti ya kampuni hiyo imeamua kusaidia kituo hicho kwa kuchangia uboreshaji wa vyumba vya kulala vya wazee hao.

"Tulipokea ombi la kufikiria kusaidia kituo hiki kwa njia mbalimbali. Tunafahamu kituo hicho kilianzishwa miaka mingi iliyopita, hivyo baadhi ya miundombinu na vifaa vinahitaji maboresho ndiyo maana uongozi uliamua kuchangia magodoro 50.

"Kama sehemu ya AngloGold Ashanti, moja ya maadili ya biashara ya GGML, ni kwamba jumuiya na jamii tunakofanyia kazi lazima ziwe na maisha bora. Tunatumaini magodoro haya yataboresha maisha ya wazee zaidi ya 50 wanaoishi hapa," alisema.

Msimamizi wa Kituo cha Wazee cha Bukumbi, Jonas Tarimo, alishukuru GGML, kwa msaada huo na kuongeza kuwa utasaidia kutoa huduma za malazi bora na salama kwa wazee wa kituo hicho.

"Hiki ndicho kituo pekee cha kuishi wazee kilichopo karibu na mikoa ya Geita na Mwanza. Tumebahatika kuungwa mkono na Mgodi wa Dhahabu wa Geita ndiyo maana tunaona wakazi wengi wanafurahia msaada huu," alisema.

GGML, imekuwa kinara wa uwekezaji katika jamii tangu ilipoanzishwa mwaka 2000, huku vipaumbele vikubwa vikiwa ni miradi ya afya, elimu, maji, barabara, miradi ya maendeleo na miradi mingine ya kijamii inayolenga kuboresha ustawi wa jamii inayowapokea.

Mapema mwaka huu, kampuni ilitangazwa kuwa mshindi wa jumla wa kampuni zilizofanya vyema katika sekta ya madini nchini kwa mwaka wa 2020/2021 baada ya kushinda tuzo za uwajibikaji wa kampuni kwa jamii, mazingira, usalama, mlipakodi bora na maudhui ya ndani.

# Watoto 712,000 kuchanjwa polio

**Na Lilian Lugakingira,** BUKOBA

JUMLA ya watoto 712,361 wenye umri wa chini ya miaka mitano wanatarajiwa kupatiwa chanjo ya ugonjwa wa polio katika Mkoa wa Kagera wakati wa kampeni ya siku nne kuanzia leo.

Kutolewa kwa chanjo hiyo kunalenga kudhibiti maambukizi ya ugonjwa huo kutokana na kuthibitika kuwapo kwa mlipuko katika baadhi ya nchi jirani.

Akitoa taarifa ya kufanyika kwa kampeni hiyo, Mratibu wa Chanjo wa Mkoa wa kagera, Zabron Segeru, alisema chanjo hiyo ni ya awamu ya pili, awamu ya kwanza ilitolewa mwezi Mei mwaka huu.

Segeru, alisema wamekuwa wakitoa chanjo hiyo karibu kila siku katika vituo vyao vya kutolewa huduma za afya lakini kwa sasa kutokana na kuwapo kwa mlipuko katika baadhi ya nchi zinazoizunguka Tanzania, hata kama mtoto alikwishapata chanjo hiyo, inabidi achanje tena ili kuongeza kinga.

Alitumia fursa hiyo kuwataka wananchi wenye watoto wenye umri chini ya miaka mitano, kutoa ushirikiano wakati wa kampeni hiyo ili kuhakikisha watoto wote wa umri huo wanachanjwa.

"Kuna watoto inawezekana watakuwa wamelazwa hospitalini, hawa watachanjiwa huko, lakini wazazi wengine wanaweza kuwawahisha katika vituo vya kutolea huduma, na ambao watashindwa tutawafuata huko iwe shuleni, sokoni, nyumbani na sehemu yoyote yenye mkusanyiko," alisema.

Baadhi ya wazazi waliozungumzia kampeni hiyo, walitoa rai kwa wananchi wenzao kuitikia kwa wingi ili kuhakikisha kinatengenezwa kizazi cha watu wasio tegemezi kwa kuwa mtoto akishapata ugonjwa wa polio anaweza kupooza.

"Kwahiyo kila mzazi ana wajibu wa kuhakikisha mtoto wake mwenye umri huo anachanjwa ili kuepusha madhara ambayo yakitokea yatasababisha familia kuwa na mzigo mkubwa wa kumhudumia mhusika mpaka mwisho wake wa maisha, kwa sababu akishakuwa mlemavu hawezi kujihudumia" alisema Jovin, mmoja wa wananchi mkoani hapa.

Kwa mujibu wa Mratibu wa Chanjo wa Mkoa, madhara makubwa yanayosababishwa ugonjwa wa polio ni kupooza mwili na kumsababishia mhusika kupata ulemavu wa kudumu.

HABARI KITAIFA

# Balozi ataja fursa Brazil

**Na Elizabeth Zaya**

BALOZI wa Tanzania nchini Brazil, Prof. Adelarous Kilangi, ametaja fursa mbalimbali zinazopatikana nchini humo na kuwataka Watanzania kuzitumia kujiletea maendeleo na taifa kwa ujumla.

Akizungumza na waandishi wa habari kwa njia ya mtandao akiwa nchini humo, alisema zipo fursa na sekta mbalimbali ambazo ni muhimu kwa Watanzania kuzichangamkia, na kwamba ubalozi umeshafanya mazungumzo na wadau wanaohusika kwenye maeneo hayo kwa lengo la kuhakikisha wanatekeleza jukumu lao la kuimarisha diplomasia ya uchumi.

Alitaja baadhi ya sekta ambazo tayari ubalozi umeona fursa hizo kuwa ni pamoja na kilimo, mifugo na uvuvi, nishati na gesi, utalii, viwanda na biashara, michezo na lugha ya Kiswahili na sekta ya afya.

Alitaja fursa kubwa za kilimo zipo kwenye maharagwe ya soya, mtama na mahindi ya njano.

"Pia wakulima wetu Tanzania watapata fursa ya kujifunza matumizi ya teknolojia na utaalamu wa kisasa katika kilimo hicho cha soya, mtama na mahindi ya njano," alisema Balozi Kilangi.

Alisema, eneo lingine lenye fursa ni la zana za kilimo na nchi ya Brazil ni miongoni mwa zinazozalisha na bora kulinganisha na zinazotengenezwa maeneo mengine.

"Ubalozi ulitembelea maonyesho ya zana hizo mwaka huu na kuzungumza na kampuni kadhaa ikiwamo zana za kusafisha, kung`oa visiki, kulima, kupanda, kupalilia, kumwagilia, kuvuna, kupaki, kwa hiyo Watanzania watapata fursa ya kunufaika na hili," alisema Balozi Kilangi.

Alitaja pia, fursa ya utengenezaji wa mbolea ambayo ubalozi ulifanya ziara ya kuyatembelea baadhi ya kampuni ambazo zinazalisha bidhaa hiyo na kugundua kuwa malighafi kubwa inayotumika kutengeneza mbolea hiyo ni madini ya gypsum.

Balozi Kilangi, alisema eneo jingine ambalo Watanzania watanufaika kutoka Brazil ni la umwagiliaji, ambalo nchi hiyo imepiga hatua kubwa na kwamba tayari wamewasiliana na baadhi ya kampuni ambazo zitakuja Tanzania kutekeleza baadhi ya miradi kwa kutumia teknolojia ya kisasa.

Kwenye uvuvi, alisema fursa zilizobainishwa katika sekta hiyo ni ufugaji wa ng`ombe na upatikanaji wa mbegu bora ya mifugo hiyo pamoja na dawa zao, usindikaji wa nyama na maziwa na kwamba wanafanya mazungumzo na kampuni mbalimbali yaani kuwekeza nchini katika eneo hilo.

Alisema, eneo ambalo wanazungumza na wawekezaji ni katika mafuta ya ethanol, kama njia ya kuongeza uzalishaji wa mafuta kwa lengo la kusaidia kushusha gharama zake kwenye bidhaa hiyo.

"Pia, tuligundua kuwapo kwa teknolojia itokanayo na kuozesha mabaki ya chakula, kwa hiyo tukaona kwamba ipo fursa ya kujifunza teknolojia hiyo kwa wadau wengi Tanzania ikiwamo wakulima wadogo kwa sababu kwa kutumia mimea ya mashambani, badala ya kuchoma watatumia kuzalisha nishati na mabaki yatatumika kama mbolea ya asili," alisema.

Kwenye utalii, alisema wamewasiliana na kampuni tatu kwa ajili ya vivutio na kwamba hitaji ni usafiri wa moja kwa moja kutoka nchini humo.

Alisema, wamefanya mawasilino na wenye viwanda na kuangalia uwezekano wa kuanzisha mahusiano ya kuwawezesha wahusika kupata mafunzo nchini Brazil katika chuo kikubwa cha utafiti wa viwanda na ujenzi wa nyumba nchini humo.

# Akiri mahakamani kujifanya Rais Samia

**Na Grace Gurisha**

MJASIRIAMALI Nickson Mfoi (20), amekiri mahakamani kutumia akaunti ya Facebook yenye jina la Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan na kujipatia Sh. 40,000 kwa njia ya udanganyifu.

Mfoi alikiri hayo jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Richard Kabate wakati Wakili wa Serikali, Ashura Mzava, akimsomea mshtakiwa maelezo ya awali, baada ya upelelezi wa kesi hiyo kukamilika. Mshtakiwa, anadaiwa kujiwasilisha kuwa yeye ni Rais Samia na kutumia laini ambayo haijasajiliwa.

Pia mshtakiwa huyo alikiri kwamba kati ya Septemba, 2021 ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa nia ya kulaghai umma alijiwasilisha kama Rais Samia Suluhu Hassan kupitia akaunti yake Facebook.

Alidai kupitia mtandao huo alijipatia Sh. 40,000 na pia Oktoba 2 alikutwa akitumia laini ya simu ambayo awali ilikuwa inamilikiwa na Getness Jackson kwa madai kwamba alipewa na mtu anayesajili laini.

"Ni kweli hii akaunti ya Facebook nilikuwa naitumia mimi, niliuziwa, lakini yaliyokuwa yakiendelea humo mimi siyajui na ni kweli nilikuwa natumia simu ambayo haijasajiliwa kwa kidole changu," alidai Mfoi.

Alikiri kwamba Septemba, 2021 alikamatwa na askari katika hoteli ya Malaika mkoani Mwanza na alipopekuliwa alikutwa anamiliki simu moja na laini iliyosajiliwa kwa jina la Jackson bila kutoa taarifa kwa mtoa huduma na kukamatwa.

Alidai wakati anahojiwa na askari, alikiri kutenda makosa yote na Agosti 4, 2021 alipelekwa mahakamani kujibu mashtaka yake. Mshtakiwa huyo baada ya kukiri makosa hayo, alipewa jalada la mahakama kwa ajili ya kusaini na Hakimu Kabate aliahirisha kesi hiyo hadi Septemba 7, 2022 kwa ajili ya kupokea vielelezo vilivyotajwa kutokana na kukubali kukutwa navyo na kuvitumia.

Mshtakiwa alirudishwa rumande kwa kushindwa kutimiza masharti ya dhamana ya kuwa na mdhamini mmoja mwaminifu na mwenye kazi ambayo inaaminika akiwa na Kitambulisho cha Taifa.




Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Benki ya Biashara Tanzania (TCB), Moses Manyatta (kulia), akikabidhi msaada wa mifuko 500 ya saruji kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Sumbawanga, Lightness Msemo, Mjini Sumbawanga hivi karibuni, kwa ajili ya kukamilisha ujenzi na kufanya marekebisho kwenye shule zenye uchakavu katika halmashauri hiyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TAKUKURU kusikiliza kero kila Alhamisi ya mwisho wa mwezi

**Na Waandishi Wetu**

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), imekuja na mikakati ya utaratibu wa kutenga siku maalumu ya kusikiliza malalamiko ya wananchi kwa kuwafuata maeneo mbalimbali chini ya mpango 'TAKUKURU inayotembea' kila Alhamisi ya mwisho wa mwezi kwa ajili ya kusikiliza kero.

"Tunaendelea na ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo pamoja na utaoji huduma katika taasisi za serikali ili kuhahakikisha wananchi wanaridhika na huduma zinazotolewa na serikali, pia wasisite kutoa taarifa zozote za rushwa katika ofisi zetu," alisema Kaimu Mkuu wa TAKUKURU Kinondoni, Ismail Seleman.

Alisema hayo wakati akitoa taarifa ya taasisi hiyo kubaini tatizo la urejeshaji mikopo ya asilimia 10 kwa makundi maalum ya vijana, wanawake na wenye ulemavu katika Manispaa ya Kinondoni.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, Seleman alisema walibaini hayo katika uchambuzi wa mifumo miwili kuangalia mianya ya rushwa kwenye usimamizi.

Alisema walibaini kuwa mikopo iliyotolewa kwa mwaka 2021/2022 ni Sh. 6,735,574,946 huku kiasi kilichorejeshwa ni Sh. 1,119,877,500 sawa asilimia 16.63 ambacho hakiwiani na kiwango cha mkopo.

"TAKUKURU ilibaini kuwapo changamoto ya urejeshaji wa mikopo. Baada ya uchambuzi huo tulipendekeza kuwa Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni waongeze juhudi katika ufuatiliaji ili kuhakikisha fedha zilizokopeshwa zinarejeshwa serikalini ili kusaidia walengwa wengine waweze kukopa," alisema.

Seleman alisema pia walibaini jumla ya taarifa 114 zinazohusu vitendo vya rushwa ilikuwa ni 47 na zinazohusu masuala ya rushwa 67.

"Katika taarifa 47 zinazohusu vitendo vya rushwa, tumefungua majadala 36 yanaendelea kwa uchunguzi wa kina na 11 yamekamilika yapo ofisi ya taifa kwa mashtaka," alisema.

Pia alifafanua kuwa mchanganuo wa kisekta wa malalamiko 114 kwa kila taasisi kwenye mabano ni; asasi binafsi (40), TAMISEMI (27), ardhi (4), polisi (12), mahakama (13), Wizara ya Elimu (4) na malalamiko (14) yaliyohusu mtu mmoja mmoja.

"Kipindi cha karibuni kesi mpya zimefunguliwa nne katika Mahakama ya Wilaya ya Kinondoni na kufanya jumla ya kesi 17 zinazoendelea mahakamani," alisema.

**■Imeandikwa na Loyce Cyriacus (SJMC) na Sabina Ntobi (TUDARCo)**

# RC Chalamila aagiza taasisi zilipe ankara, kukatiwa maji

**Na Restuta Damian,** BUKOBA

MKUU wa Mkoa wa Kagera, Albert Chalamila, ameiagiza Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira katika Manispaa ya Bukoba (BUWASA) kulipa ankara za malipo taasisi zote zinazodaiwa maji na kama zikishindwa kulipa, zikatiwe huduma hiyo.

Alitoa agizo hilo jana alipozungumza na uongozi wa BUWASA ambao unaotoa huduma ya maji kwa wananchi walioko Mtaa wa Majengo katika Kata ya Kashai, Manispaa ya Bukoba mkoani humo.

"Kama kuna taasisi yoyote ya serikali inadaiwa ipeni notisi leo, weka nukuu ya vifungu vyako juu ya uendeshaji na baada ya muda, mkate maji, katika hili huwa sidanganyi," alisema.

Chalamila alielekeza kuwa baada ya kukatiwa maji, hakuna taasisi itakayosumbua kulipa na huduma haitarudishwa mpaka watakapolipa deni lao.

"Hakuna mtu atakayesumbua na baada ya hapo mimi nitajua namna ya kuwasiliana na mamlaka zao ili madeni yalipwe," alisema.

Chalamila alisema makusanyo yanayopatikana kwenye mamlaka hiyo, yanaisaidia kujiendesha yenyewe kama watoa huduma kwa wananchi.

Alisema ili kuendelea kustawi na kufanya huduma kuwa bora, ni lazima ufuatiliaji wa miradi uwe na uhakika na vifaa vinavyotumiwa.

Mkurugenzi wa Mamlaka hiyo, John Sirati, alisema kuwa mbali na mitaa tajwa huko juu, huduma ya maji inatolewa kwenye kata 14 zilizoko Manispaa ya Bukoba.

Aliongeza kuwa uzalishaji wa maji ni lita za ujazo milioni 18 kwa siku kutoka kwenye chanzo kikuu cha Ziwa Victoria na mahitaji kamili ni lita za ujazo milioni 13.

"Kwa siku tunazalisha lita za ujazo milioni 18 ambazo zinatoka kwenye chanzo chetu kikuu ambacho ni Ziwa Victoria, tuliweka eneo la Bunene na mahitaji ya wateja ni lita za ujazo milioni 13," alisema Sirati.

Kaimu Katibu Tawala wa mkoani Kagera, Projestus Rubanzibwa, alisema ni vyema taasisi za umma kuwasilisha taarifa za utekelezaji kila robo mwaka ili kufahamu kinachoendelea.

## Ajali nyingi barabarani ni makosa kibinadamu

**Na Fatuma Athumani,** TUDARCo

JESHI la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani limesema asilimia 90 ya ajali za barabarani zinazotokea nchini zinasababishwa na makosa ya kibinadamu.

Ofisa Mkaguzi wa Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani, Dumu Mwalugenge, alibainisha hayo jana alipohojiwa kwenye kipindi cha Kumepambazuka kinachorushwa na Radio One.

Alisema vyanzo vya ajali ni uendeshaji magari wakati dereva amelewa, ubovu wa magari na hali mbaya ya hewa.

"Kama unaona kuna hali ya ukungu, mvua kubwa, barabarani ni bora upaki gari pembeni mpaka pale hali itakapokua sawa, au kuendesha gari wakati umemeza dawa zinazokufanya ujisikie uchovu na kuendesha gari huku una msongo wa mawazo, ni hatari," alifafanua Mwalugenge.

Alisema kuna umuhimu wa kurekebisha sheria za usalama barabarani kwa kuongeza masuala ya kiteknolojia, ukaguzi wa magari kwa kutumia mitambo maalum, kuweka kamera barabarani na doria.

Mwalugenge aliwataka wamiliki na madereva kukagua magari kabla ya kuendesha kwa kuangalia mikanda, umeme wa gari, maji na breki.

"Hakuna chombo cha moto kitaruhusiwa kuingia barabarani kama kina hitilafu, ili kujiepusha kukamatwa kwa sababu tutafanya ukaguzi mkali na ukikutwa unakosa,




Mwenyekiti wa Jumuiya ya Khoja Shia Ithanasheri Tanzania, Mohamedraza Dewji, akizungumza na waandishi wa habari, wakati wa kambi ya siku tatu ya kupima afya na maradhi yasiyoambukiza iliyoandaliwa na jumuiya hiyo, katika viwanja vya Mnazi Mmoja, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Jumuiya yasaidia matibabu ya akili

**Na Mwandishi Wetu**

NUSU ya magonjwa ya akili duniani yanaanza katika umri wa miaka 14 na mengi hayabainiki wala kutibiwa, suala linaloweka mustakabali wa vijana wengi njiapanda katika nchi zinazoendelea.

Hayo yalibainishwa katika kambi ya siku tatu ya kupima afya na maradhi yasiyoambukiza katika Viwanja vya Mnazimmoja jijini Dar es Salaam iliyoandaliwa na Jumuiya ya Khoja Shia Ithnasheri.

Mwenyekiti wa Jumuiya hiyo Tanzania, Mohamedraza Dewji, alisema jana kuwa imani potofu na unyanyasaji wa kijinsia katika maisha ya binadamu, huwatesa wananchi walio wengi na kushindwa kumudu gharama za matibabu na kupelekea kuongezeka kwa idadi kubwa ya magonjwa ya akili.

Mohamedraza alisema msongo wa mawazo ni mvurugano katika mkwamo wa uhusiano, uchumi na mengineyo ambayo huwakumba mtu mmoja kati ya wanne kwa nyakati tofauti.

Alisema ugonjwa wa msongo wa mawazo ni chanzo namba mbili kwa vifo kwa vijana wenye umri kati ya miaka 19 hadi 29 na kuelezea kuwa asilimia 75 ya watu wanaokabiliwa na ugonjwa huo katika nchi zinazoendelea, hawapati matibabu ya uhakika.

"Kwa kweli hali ya maradhi ya akili inazidi kuwaathiri watu wengi na inadaiwa kuwa watu milioni 350 duniani wameathirika na msongo wa mawazo na kwa waathirika wengi hunyanyapaliwa kwa kuwa na ugonjwa huo na hali hiyo huzuia watu wengi wenye maradhi hayo kupata msaada," alisema Mohamedraza.

Mwenyekiti huyo pia aliishauri jamii jinsi ya kupambana na msongo wa mawazo kwa kuacha kunywa pombe, kula chakula kingi kupita kiasi, kukaa kwenye runinga au kompyuta mpakato kwa muda mrefu, kujitenga na marafiki, familia au kula vidonge au kulala sana na kujishughulisha wakati wote na kupayuka, kubwata au kufoka.

Oktoba 7 ya kila mwaka nchini kunafanyika maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Afya ya Akili, ikitumiwa na wadau wa afya na Shirika la Afya Ulimwenguni (WHO) kuhamasisha kuhusu ufahamu wa magonjwa hayo, tiba na hata kinga.

Ukurasa 13




Tukidekezana kwa mambo ya msingi hatutafika



**KUSUASUA KIWANDA CHA CHAI MPONDE.. Ziara ya Komredi Chongolo yawasha moto ghafla yapata uhai, waziri na RC watinga**

Ukurasa 12



# Asimulia TASAF ilivyowafanyia maisha yaeleweke kwa plau cherehani, baiskeli

**Na Shaban Njia, MBOGWE.**

SERIKALI ilianzisha Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) kuanzia mwaka 2000, ikinuia kutokemeza umasikini, pia ukisadia ajenda ya ugatuaji wa madaraka nchini .

Katika kipindi cha mwaka 2009/2012 Tasaf ilifaya majaribio uhawilishaji fedha kwa tasilimu kwa masharti (CCT) katika Wilaya za Kibaha, Bagamoyo na Chamwino za Tanzania bara na tathimini yake, yalileta matokeo ya mafaniko makubwa katika sekta za afya, elimu, na kuongezeka kwa rasilimali za kaya.

Utekelezaji awamu ya kwanza yalikuwa ni kuziwezesha kaya masikini kuongeza kipato na fursa za kujikimu. Hivi sasa, katika wilaya ya Mbogwe mkoani Geita, Tasaf imeonyeha mafaniko makubwa kukuza uchumi wa wananchi hasa waliopo katika maeneo pembezoni, kutokana na fedha walizopatiwa, wameanzisha mradi chanya wa maendeleo; kilimo, ufugaji kuku, bata na wanyama.



Mnufaika wa TASAF Rucia Gh'oni, mkazi wa kijiji cha Mwabukwalule Halmashauri ya Mbogwe, mkoani Geita ambaye ni mjane, akiwa ameshika Plau aliyonunua Sh.150,000 kutokana na kilimo cha zao la mpunga, kwa kutumia mfuko wa TASAF, alipata magunia 10 ya mpunga aliyolima. **PICHA: SHABAN NJIA.**

### CHEREHANI NA BAISKELI

Kwa Kashindye Kube (41), mkazi wa kijiji cha Mlale kata ya Ushirika, wilayani huko sasa anajinasibu kuwa miongoni mwa wanufaika wa ruzuku akipokea Sh.54,000 kila mwezi anazotumia kwa kushirikiana na mkewe kupanga matumizi, ili kuhakikisha zinawanufaisha pamoja.

Anasimulia, alipopata fedha hizo, akazielekeza kwenye kilimo chenye tija na alipouza mazao akanunua baiskeli ya kumpeleka mkewe kuhudhuria kliniki, kama sehemu ya kupambana na vifo vya wajawazito na watoto.

Kube anasimulia, kabla ya kuwepo TASAF alitumikia vibarua mashambani akishirikiana na mkewe, Rusia Nzumbi na fedha walizozipata walitumia kuendesha maisha ya familia, akikiri zilikuwa hazikidhi mahitaji.

"Mimi na mke wangu (sasa) tunapokea fedha za TASAF, tunakaa pamoja na kupanga nini cha kufanya chenye tija na ndio maana mpaka sasa tumefanikiwa kupiga hatua katika maisha yetu na tunashamba la ekari mbili tumelima mihogo," anasimulia Kube.

Mnufaika mwingine, Clemensia Nyambae (37) anayeishi kijijini Budoda, anasema amefanikiwa kununua cherehani ya kushona nguo, kutokana na pato la TASAF, huku anahifadhi akiba kutoka ruzuku hiyo.

Anasimulia bajeti yake, Septemba mwaka 2015, alipokea Sh.36,000 na kuhifadhi Sh10,000 kwa ajili ya kununua cherehani na nyingine alizitumia kwa chakula nyumbani.

Anasema, uhifadhi wa fedha sehemu ya ruzuku ya TASAF ilifika kiasi cha Sh.150,000 na mwaka 2018 alinunua cherehani, ambayo mpaka sasa anapotoka shambani kulima bustani, huelekea kushona nguo za wateja wake na anapata fedha za kuendelea kuendesha maisha yake.

Anasema, kwa siku sasa ana uwezo wa kupata Sh.3,000 hadi 5,000 anapowashonea nguo wateja wake kwa marekebisho na kushonewa upya ni Sh.8,000.

### BWAWA LA TASAF

Masumbuko Amosi, mfugaji wa kijiji na Kata ya Ngemo Halmashauri ya Mbogwe, anasema wameondokana na adha ya kukamatwa mifugo yao na maliasili kwa kuingiza mifugo ndani ya pori la Hifadhi ya Lwamgasa na kunywesha mifugo katika vyanzo vya maji vilivyopo hifadhini.

Adha anasema hali hiyo imetoweka baada ya walengwa wa TASAF katika miradi ya ajira za muda wa kijiji cha Ngemo kuchimba bwawa kubwa la maji kwa ajili ya shughuli za kilimo cha bustani cha mbogamboga, matunda pamoja na kunyweshea mifugo yao hususani Ng'ombe.

"Niwashukuru wanufaika wa TASAF kijijini kwetu kwa kuona umuhimu wa kuchimba bwawa hili la maji ambao tunalitumia kwa matumizi ya kilimo na kunyweshea mifugo yetu, nasi tutalitunza ili lisije likajaa tope, maji yakapungua na mifugo yetu ikahangaika tena"aliongeza.

Bujiku Malulu anasema, baada ya kuchimbwa kwa bwawa hilo alilazimika kununua hekari 1.5 jirani na kuanza shughuli ya kilimo cha matikiti maji, Nyanya, Vitunguu, Mahindi, Maharage na kabechi na manufaa ameshaanza kuypata baada ya kuivisha mazao na kuuza.

Msimamizi wa bwawa hilo Fatuma Selemani ambaye ni mnufaika wa TASAF anasema, bwawa hilo walilichimba mwaka jana kuanzisha shughuli za kilimo cha umwagiliaji na kuwasaidia wafugaji wanakijiji ambao mifugo yao ilikuwa ikikamatwa hifadhini.

### MRATIBU TASAF/ MTENDAJI KATA

Ofisa mtendaji wa kata ya Buzigonzi Joseph Bahati anasema, awali wanufaika wengi walikuwa wakipokea fedha na kuzielekeza katika matumizi ya unywaji wa pombe lakini baada ya kuanza kuwafuatilia na kuwapatia elimu ya ujasiriamali kila mnufaika anashughuli ya kumwingizia kipato.

Nae Mwenyekiti wa kijiji cha Shibutwe Elikana Bunzali anasema, wamekuwa wakishirikiana na Watendaji wa kata,vijiji na waratibu wa TASAF katika kuhakikisha wanufaika wote wanazitumia fedha katika shughuli muhimu za kuwaingizia kipato ili wasiendelee kuwa tegemezi hapo baadae.

Kwa upande wake, Mratibu wa TASAF Mbogwe, Mercy Joseph anasema, wameweka utaratibu wa kuwatembelea wanufaika ili kujua wanazitumia vipi fedha za ruzuku wanazozipokea na wamebaini wengi wamezielekeza katika shuguli za kilimo, ujasiriamali na ufugaji.

UCHUMI

KUSUASUA KIWANDA CHA CHAI MPONDE..

# Ziara ya Komredi Chongolo yawasha moto ghafla yapata uhai, waziri na RC watinga

- Tangu izimike 2013, yaanza tena uzalishaji jana
- Ni tabasamu la ajira, hadi mashambani Bumbuli

**Na Mary Geofrey**

KUNA simulizi ndefu kuhusu Kiwanda cha Chai Mponde. Ni wastani wa miaka 21, ujumbe maalum wa Tume ya Rais ya Kurekebisha Mashirika ya Umma (PSRC), ulizuru mahali hapo kusimamia ufufuaji wake chini ya hisa kuu ya sekta binafsi.

Ni katika kipindi ambacho miradi ya umma, vikiwamo viwanda mbalimbali, vilikuwa katika mapito ya ubinafsishaji upya, kwa wawekezaji binafsi PSRC.

Kwa mujibu wa utaratibu huo, ubinafsishaji ulikuwa na sura kuu tatu; kuuzwa kwa asilimia zote kwa shirika la umma au 'SU' lililokwama kabisa; pia hisa kubwa zaidi ya asilimia 50 kwa mwekezaji binafsi na zilizobaki wagawana hisa serikali na umma.

Pia, kuna sura ya ubinafsishaji kwa hisa zote za 'SU; miliki yake kuhamishiwa wafanyakazi kama ilivyofanywa kwa Kiwanda cha Uchapaji cha Taifa (KIUTA) na ya mwisho, taasisi kuazimwa kwa muda maalum, kama ilivyowahi kutokea kwa Shirila la Reli Tanzania (TRC), kisha mkataba ukaharibika.

Ikirejewa kiwandani Mponde, ahadi iliyokuwapo kutoka kwa mmiliki binafsi miaka 21 iliyopita, alikuwa anaendelea na maboresho ya msaada, baada ya muda mfupi wangeingia mazungumzo na wananchi juu ya hatima ya milki ya uzalishaji huo.

Ni wakati huo kukashuhudiwa mazingira baridi ndani ya milima ya Bumbuli, Lushoto kunakopatikana kiwanda cha Mponde wakulima wamepanawirisha na kumea mashamba ya chai.

Ni nakshi isiyo tofauti na penye mashamba ya chai Tukuyu, wilayani Rungwe na viwanda vyao vya Katumba jirani na Tukuyu mjini, pia Mwakaleli iliko sasa Halmashauri ya Busokelo, nacho kilikwama wakati fulani, zote mkoani Mbeya.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Ajira, Vijana na Watu Wenye Ulemavu) Profesa Joyce Ndalichako (wa pili kushoto), alipotembelea na kukagua kiwanda cha Chai Mponde Agosti 16, mwaka huu kukagua ukarabati wakati wake. Wa kwanza kulia ni Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Omari Mgumba na katikati ni Mkurugenzi Mkuu wa WCF, Dk. John Mduma

Simulizi hiyo ya kuzalisha chai inafika hata mikoa jirani na Mbeya, ambayo ni Njombe na Iringa au hata kufika nchi jirani katika wilaya ya Thyolo, umbali mfupi kutoka jijini Blantyre, Malawi.

Ni bahati mbaya simulizi ya kukifufua kiwanda hicho cha Mponde imekuwa endelevu hata wakati fulani kutua Bungeni, lakini ufufuaji wake ukidumu kitendawili kigumu.

Sasa Chama cha Mapinduzi (CCM) kilichoshika hatamu za uongzozi kimeamua 'kushikia bango' majibu yapatikane chini ya operesheni maalum ya mtendaji wake mkuu, Katibu Mkuu, Komredi Chongolo.

**PICHA KAMILI**

Kimsingi, Kiwanda cha Chai cha Mponde kinafanya kazi ya uzalishaji kikisindika majani mabichi ya chai katika Halmashauri ya Bumbuli, kikitegemewa na wakulima wadogo wa chai wapatao 5,000.

Wakulima hao wanakitegemea kiwanda hicho kama soko la majani mabichi ya chai kutoka mashambani mwao yao, lakini kwa takribani miaka 10 uzalishaji ulisimama kutokana na mgogoro uliojitokeza mwaka 2013, hata kiwanda hicho kikafungwa..

Hiyo ni baada ya mwekezaji aliyefahamika kama Umoja wa Wakulima wa Chai Usambara (UTEGA - Usambara Tea Growers Association) kukiuka masharti ya ubinafsishaji na serikali kujiridhisha kulikuwapo kasoro katika namna ya kukiendeleza kiwanda hicho.

Mnamo 2021 miaka minane baadaye, serikali iliruhusu rasmi kiwanda kuanza uzalishaji na timu ya wataalamu ikaingia kazini kuboresha mitambo kiwandani, ili kazi ianze haraka wakiwa na mkakati wa kujenga kiwanda kipya katika eneo hilo.

Sasa Mkuu wa Mkoa Tanga,Omari Mgumba anaweka rasmi, kuanza kazi jana Septemba Mosi, baada ya kujiridhisha na hatua za ujenzi, ukarabati na maandalizi kukamilika kwa asilimia 96, ili kazi ianze, kikiwa kwenye majaribio kwa miezi mitatu.



Sehemu ya nje ya mandhari ya Kiwanda cha Chai Mponde, Lushoto. **PICHA ZOTE: MAKTABA.**

**UGENI WA CHONGOLO**

Katibu Mkuu CCM), Daniel Chongolo, akafanya ziara mkoani Tanga, moja ya mambo akakutana nayo, ni mradi huo wa kiwanda cha Mponde. Hapo 'anapigilia msumari' akiahidi kuusimamia mradi huo hadi anahakikisha uzalishaji na mauzo yake yanafanyika.

"Hivi si kuna watu hapa wamekopa mbolea? Si kuna ambao wameanza kukatakata chai naziona hapa? Si mwezi mmoja tutakuwa na chai ya kuchuma? Tutaipeleka wapi, tukamwage?... Hapana! Mwezi wa tisa kiwanda kikifunguliwa kianze kupokea na kuchakata chai za wananchi badala ya kufanya majaribio.

"Mwezi wa 12 iwe ni kuzindua kwa kukata utepe na huku wananchi wakiendelea kunywa chai na sio vinginevyo. Haiwezekani kila siku tunaenda mbele tunarudi nyuma, ndio maana nimekuja," anasisitiza Chongolo.

Hapo ana ufafanuzi wake, akiwa Msaidizi wa Mwenyekiti wa chama, Rais Samia Suluhu Hassan, ana wajibu wa kuhakikisha mambo yanaenda sawa kwa mujibu wa ilani ya uchaguzi wa chama chao kinachotawala, jambo hilo ni moja ya jukumu lake kusimamia kupitia kwa watendaji waliopewa jukumu hilo.

Hapo anafafanua ilani hiyo ya mwaka 2020 hadi 2025, anataja chai imo katika orodha ya mazao ya kimkakati na kwa sasa inazalishwa tani 37,000 lakini serikali imejipanga kuongeza hadi kufika tani 60,000 mwaka 2025.

"Nitakuwa wa mwisho kuacha mzembe kuendelea kutukwamisha kwenye mambo,tutamshauri mwenye mamlaka (Rais Samia) kuchukua hatua, ili tuachane naye tusonge mbele," anatamka Chongolo kwa kung'aka na kuongeza " Kwa kuwa tupo Watanzania wengi wenye dhamira ya kumsaidia Rais Samia kwenda mbele kwa kasi, wale watakaotukwamisha, wala haitakuwa gharama kuwashusha,".

**RC MGUMBA WA TANGA**

Mkuu wa Mkoa Mgumba, anataja ratiba rasmi, ni kuanza uzalishaji ili kuwezesha wananchi wanaovuna chai waanze kuchakatwa kiwandani na Desemba ijayo, uzalishjaji rasmi utachukua nafasi.

Hata hivyo katika ratiba hiyo ya majaribio, Mgumba ana pingamizi lake kwa uzinduzi wa Desemba , akiwa na sababu wananchi wa Halmashauri ya Bumbuli kiliko kiwanda, walipatiwa mkopo kutoka benki ya NMB zaidi ya Sh. milioni 120 walizonunulia mbolea na kuweka na wako katika hatua za kuvuna.

**WAZIRI NDALICHAKO**

Siku sita baada ya agizo la Chongolo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, (Kazi, Ajira, Vijana na Watu Wenye Ulemavu), Profesa Joyce Ndalichako, naye akakitembelea kiwanda hicho, kufuatilia hatua za kuanza uzalishaji.

"Kimsingi kiwanda kimekamilika kwa asilimia 95, nimefanya ukaguzi kwenye eneo la kupokea na kuchambua chai, eneo la kuchakata

'processing', eneo la kuangalia viwango na ubora 'grading', eneo la Karakana, Tanuri

la kufua joto 'boiler' na kote huko kumekamilika," anafafanua.



Katibu Mkuu wa CCM, Daniel Chongolo.

Anasema wao wizara, baada ya kupokea maelekezo walikaa na Katibu Mkuu, pia na Watendaji Wakuu wa Mifuko ya Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF) ambao ndio wawekezaji wakuu kiwandani kuona namna bora ya kuanza utekelezaji mara moja.

"Kulikuwa na baadhi ya vifaa ikiwemo mabomba ya kutolea mvuke na nyavu za kukaushia chai ambavyo vilihitajika ili kukamilisha hatua za uzalishaji." Anafafanua.

Anasema Kiwanda cha Chai Mponde kina sura ya kuwa kiwanda cha kisasa na kitakuwa na uwezo wa kuchakata tani 5,800 kwa saa na lengo lake ni kufikia tani 16,000.

"Kwa siku wakulima watauza kilo 52,000. Naamini kwamba kiwanda kitaenda kuinyanyua Halmashauri yetu ya Bumbuli na kuboresha maisha ya wananchi," anasema Profesa Ndalichako, katika ziara aliyoambatana na Mkuu wa Mkoa Mgumba na Mkuu wa Wilaya ya Lushoto.

Pia walikuwamo Kalist Lazaro na Mkurugenzi Mkuu wa WCF, Dk. John Mduma, aliyemwakilisha Mkurugenzi Mkuu wa PSSSF, Marco Kapinga, Mwenyekiti wa Bodi ya Kiwanda hicho, Anselim Peter, Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Chai na watendaji wengine wa kiwanda.

Waziri anasema kiwanda hicho kitatengeneza ajira za moja kwa moja 79 na zingine 100 hadi 200 kulingana na msimu wa kilimo.

**WANANCHI WANACHEKELEA**

Ni hatua ambayo kwa wakulima wa chai nao wameonyesha matumaini kutoka kwa hatua na ziara hizo, wakati mashine za kuchata chai zilikuwa zikisubiriwa kuwashwa.

"Mimi sasa nina matumaini makubwa kwamba kiwanda hiki kitaanza kazi, nimeona mabadiliko makubwa yamefanyika, nimshukuru sana Rais wetu, Mama Samia

kwa kazi kubwa hii iliyofanyika." Anasema Mkulima wa Chai Bumbuli Mzee Said Ngereza.

Amina Sufiani, anasema ujio wa viongozi umeleta matumaini makubwa kwao na matarajio yao ni kuwashwa tu kwa mashine hizo na sio vinginevyo.

"Sisi kama wakulima tumejipanga kwenda shambani, pelekeni salamu kuwa serikali

inatufungulia kiwanda nasi tuko tayari.," anasema mkulima mwingine.

TAFAKURI YA MLALAHOI

# Tukidekezana kwa mambo ya msingi hatutafika




MIAKA ya nyuma tukiwa wadogo, tulizoea kudeka kwa wazazi, ingawa wakati mwingine deko zetu ziliishia kwenye kichapo. Mathalan unamdekea baba yako eti akununulie keki ndipo ule ugali.

Unamdekea baba yako akununulie mwanasesere wa gari ndipo uende shuleni. Wapo wazazi waliokubali deko na kutimiza mahitaji ya mdekaji, naye akafanya alivyotaka, huku mzazi akiendelea kumdekeza.

Lakini, kama nilivyosema awali,walikuwapo wazee waliolazimika kuwa wanoko kutokana na hali halisi ya maisha, kwamba hana kitu na amejitahidi uwe ulivyo, ila sasa fadhila zako ni kumdekea, huendi shule ila kwa masharti. Kichapo kilikuhusu walahi!

Watoto ni kawaida yao kudeka, hata kwa mambo waliyofanyiwa kwa faida yao, mathalan kusomeshwa, unanunuliwa sare mpaka viatu na unapewa vifaa na ikibidi upelekwe kwa chombo cha moto na unafika wakati unakataa tena kwa masharti.

Mtoto hajui kwanini anapelekwa shule na badala yake anadhani anaonewa au anateswa kuamshwa asubuhi na kuogeshwa, wakati mwingine maji ya baridi anaona kama wazazi wanamtesa, lakini kumbe hajui anaandaliwa mustakabali mwema.

Lakini, wengi kama si wote baadaye wanapokua na kujitegemea, ndipo huwaona wazazi kama waliofanya kitu kizuri katika maisha yao, kuwasomesha na hatimaye kupata maisha mzuri na kujisimamia wenyewe! Wapo wanaoshukuru, lakini wengine hujisahaulisha.

Wanaojisahaulisha ni wale wasemao kuwa ni wajibu wa wazazi kuwasomesha na kuwatunza kwa kila kitu, kama ambavyo nao wanatarajiwa kufanya kwa watoto wao



NA JOSEPH KULANGWA
Simu: +255 713 410008
barua pepe:
jkulangwa@yahoo.com

na kwa bahati nzuri ni kama mzunguko wa maisha, kwani nao kama walivyodeka pia hudekewa.

Hali hiyo nimeshuhudia hivi karibuni wakati huu wa Sensa ya Watu na Makazi, nilipoambiwa kuwa kuna Watanzania jamii ya wawindaji, waokota matunda, warina asali; Wahadzabe wa bonde la Yaeda Chini wilayani Mbulu mkoani Manyara, eti walitoa masharti kuwa hawatahesabiwa mpaka wapewe kitoweo cha nyama ya twiga!

Naambiwa masharti hayo waliyatoa pia mwaka 2012, safari hiyo wakiomba kitoweo cha nyama ya nyani na mara zote wakitaka kisindikizwe na mazito...ndipo wasubiri makarani nyumbani kwa ajili ya kuhesabiwa, eti kinyume cha hapo, basi hawakai nyumbani watakuwa mawindoni.

Sikumbuki mwaka 2012 waliwindiwa wanyama gani wakakubali kuhesabiwa, ila mwaka huu waliwindiwa nyumbu 20 ndipo wakakubali, lakini nyakati zote hizi wakinyimwa mazito hayo... Na sijui wangepewa, tungeelewaje?

Hata hivyo, kupewa nyara za serikali tumeelewaje? Bila shaka mnajua sheria inasemaje mtu akiua nyumbu hata kwa kumgonga barabaani, atatakiwa kulipia shilingi ngapi? Ni mamilioni. Leo Wahadzabe wametingisha kiberiti nyumbu 20 wamelala. Hawa Msomero yao inawahusu ili wapumzike kuwinda.

Sakata jingine ni la mwenzetu anayetajwa kwa jina la Mapunda, Mjumbe wa Kamati ya Siasa ya Kata, anaonekana kwenye video akiapa kutoandikishwa sensa, yeye ni kwa sababu alinyimwa pesa ya Mpango wa Kusaidia Kaya Masikini- Tasaf, licha ya kuandikishwa! Huyo anapigania haki yake ya msingi, kwani ni masikini na zaidi ya hapo ni mwenye ulemavu.

Kwa kuwa alikuwa kwenye mpango, alistahili kupewa pesa yake, lakini siku ya mgawo jina lake likayeyuka na hivyo yeye kujiona kama mtu mfu, hivyo hastahili hata kuhesabiwa.

Ukitafakari haya mawili, utaona jinsi gani watu wanaweza kujiamulia mambo yao na kutoa masharti na kusikilizwa, pia wenye shida wakionewa na wenye nguvu na mamlaka kama alivyofanyiwa Mapunda.

Hata hivyo, baada ya kuchachamaa, nasikia baadaye mambo yaliwekwa sawa kwa kurudishwa kwenye mpango na hatimaye akaonekana kwenye video ya baadaye, akihamasisha watu kuhesabiwa baada ya kumalizana na wenye mamlaka yao.

Kwanini hiyo iwe ilivyokuwa? Hivi makabila mengine nayo yakiamua kuweka mguu chini ndipo yatekeleze maelekezo ya Taifa tutafika? Sensa ni kwa ajili ya nchi kujipangia mipango ya maendeleo, lakini wanaibuka watu wanadeka kama wale watoto, bila kufahamu kuwa haya yanafanyika kwa ajili ya mustakabali mwema wa nchi.

Inatufundisha nini hii? Watanzania tuwe tayari kukubaliana na mazuri ya serikali, lakini pia watu watendewe mema kulingana na mahitaji yao. Kitendo alichofanyiwa Mapunda hakikustahili na alilolifanya yeye kugoma lilistahili, ndiko kudai haki kama watu wanajifanya hawasikii. Alamsiki!

BIASHARA

HUYO NDIYE MWITA!

# Anapinga mwenye ulemavu kuomba, mfano binafsi fundi, amiliki kiwanda

**Na Magdalena Jackson, SJMC**



Mwita Marwa, Mkurugenzi wa Karakana za Walemavu Dodoma, akiwajibika kazini. **PICHA ZOTE: MAGDALENA JACKSON.**

WAKATI kundi kubwa la watu wenye ulemavu wakikaa barabarani na kuomba msaada, wapo ambao hawajatumia ulemavu wao kama kikwazo cha kutoshiriki shughuli mbalimbali za kazi za maendeleo katika jamii.

Mwita Marwa ni mwenye ulemavu wa miguu, ambaye sasa ni Mkurugenzi wa Karakana za Walemavu Dodoma, anayepatikana eneo la Sabasaba Jijini Dodoma, akishughulika na ufundi unaowahusu wenye ulemavu.

Anasema pamoja na kuwa mwenye ulemavu, hakusita kutafuta elimu ya kumsaidia kujifunza ufundi katika Chuo cha Ufundi cha Watu Wenye Ulemavu Yombo, kilichopo jijini Dar-es-Salaam, kuanzia mwaka 2004 hadi 2005 na kujiendeleza katika Chuo cha VETA Dodoma.

Kutokana na taaluma yake hiyo ya ufundi, imemuwezesha kuajiriwa katika taasisi zisizo za kiserikali kama shirika la Cheshire na Kisedet, kwa kazi ya kufundisha watu wenye ulemavu na wenye mahitaji maalum, tasnia hiyo kati ya mwaka 2011 hadi 2014.

"Nilifanikiwa kupata ajira kutoka katika shirika binafsi ambalo nilifanya nao kazi kwa muda wa miaka mitatu nikifanya kazi ya kufundisha vijana walemavu mafunzo ya ufundi. Shirika hili liliniwezesha kupata vifaa vya kufundishia na gharama za mafunzo," anaeleza.

Marwa anasema baada ya hapo, alijiajiri kwa kuanzisha karakana yake inayofahamika maalum kwa ajili ya kutengeneza vifaa vya watu wenye ulemavu na wasio na ulemavu, inayoitwa Karakana ya Walemavu Dodoma (KAWADO), eneo la Stendi ya Sabasaba jijini hapo, inayofanya kazi mpaka sasa.

Anasema, katika kazi yake amefanikiwa pia kufundisha wanafunzi zaidi ya 40, wengi kati yao wamejiajiri na wengine kuajiriwa, hatua inayomuwezesha kufahamika kwa serikali, taasisi, mashirika na jamii kwa ujumla.

Kwa mujibu wa Marwa, kufahamika huko kumemuwezesha kushirikiana na wadau kama vile Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Hospitali ya Rufani KCMC mkoani Kilimanjaro na Shirika la Ugavi wa Umeme (Tanesco), ambao wamefanikiwa kusaidia watoto wenye ulemavu zaidi ya 100 mwaka jana.

Marwa anataja baadhi ya misaada hiyo iliyotolewa kwa kushirikiana na wadau kwa watoto hao, ni pamoja na baiskeli za wenye ulemavu 10, viti vyao 10, viti vya wenye ulemavu maalum 23, fimbo kwa wasioona 150, kofia za wenye ualbino 100 na soksi zao 100.

Anasema kazi hizo, zimemfanikishha kununua kiwanja na kujenga nyumba anayoishi na familia yake, pia inamuwezesha kuwahudumia familia katika majukumu mbalimbali ya nyumbani.

Katika hilo, anatawaka wenye ulemavu kutokatishwa tamaa na hali waliyo nayo, bali waachane na vitendo vya kuomba mitaani, wajiunge kwenye vikundi wapate mikopo inayotolewa na serikali kupitia halmashauri mbalimbali zilizopo.

Pia, anawashauri ndugu zake wenye ulemavu wanapofanikiwa kupata mikopo, wahakikishe wanaifanya kazi za maendeleo, ili iwawezeshe kujiinua kiuchumi na kurejesha mikopo hiyo kwa wakati, wakiwa mbali na maisha ya kuomba mitaani.

Marwa anawataka walezi majumbani wa wenye ulemavu kutowatumia kama chanzo cha kujipatia kipato kwa kuwatembeza barabarani bali wawawezesha kujiunga katika vyama mbalimbali vya watu wenye ulemavu ili kupata msaada.

**CHANGAMOTO**

Mkurugenzi huyo anataja changamoto, ni ukosefu wa masoko ya vitu vinavyotengenezwa kiwandani kwake, kutokana na vingi vinatoka nje ya nchi na huku walemavu wenyewe wakishidwa kumudu gharama za utengenezaji vifaa hivyo.

Anasema, ukosefu wa masoko kwa vifaa anavyotengeneza katika karakana, mwenyewe akiiomba serikali kuziwezesha karakana zinazoendeshwa na wenye ulemavu waziboreshe kimiundombinu na kuhakikisha wanahimiza wananchi kununua vifaa vya wenye walemavu nchini, hali yenye msaada kwa ukuzaji soko kwa walemavu na kuinua pato la taifa.

"Tunaiomba serikali kutuwezesha walemavu kulingana na shughuli mbalimbali tunazozifanya katika jamii, kwa kutuinua pale tunapohitaji msaada, ili kufikia malengo makuu tuliyo nayo, kwani tuna mawazo mazuri na mapana yanayoweza kusaidia serikali kupunguza wimbi la watu ombaomba na tegemezi katika familia," anasema.

Hivyo, anaitaka serikali kukazia asilimia thelathini ya manunuzi ya serikali yawafikie makundi maalum ambayo ni walemavu, wazee, vijana na wanawake, kwa kununua bidhaa zinazozalishwa na makundi hayo, ili kusaidia kutatua tatizo la masoko na kuwasaidia kujikwamua kiuchumi.

Aidha, anatoa wito kwa wenye ulemavu kuachana na nyendo za kuomba, bali watumie mikopo maalum inayotolewa na serikali katika kufanya biashara kulingana na hali zao, ili waweze kurejesha mikopo hiyo kwa wakati na iwasaidie wengine.

"Tusiendelee kuwa watumwa wa kuombaomba. Jambo hili nalipiga vita sana, kwa sababu linafanya walemavu kukosa fursa mbalimbali kwa kuwa tunaonekana ni tegemezi kwa kila jambo. Ni wito wangu kwa walemavu kupiga hatua katika maendeleo kwa kujishughulisha na kufanya bidii katika kazi," anasema.

Pia, anawataka wazazi wenye watoto wenye ulemavu wasiwafiche au kuwatelekeza, bali wahakikishe wanapata elimu inayoibua vipaji na fursa, zitakazowasaidia katika maisha yao ya kila siku.

Anasema, baadhi ya watoto wenye ulemavu wanaochukuliwa na wafadhili kwa ajili ya kusomeshwa au kufanya kazi hawapewi huduma nzuri na wafadhili hao, kwa hiyo wazazi wahakikishe wanawafuatilia watoto hata wakajiridhisha wanapata huduma sahihi kutoka kwa wafadhili hao, kama walivyokubaliana.

Marwa anawakumbusha walemavu kijitokeza na kujiandaa kuhesabiwa haki ya sensa iliyoko ukingoni wahesabiwe, ili kuiwezesha serikali kupanga mikakati ya nini kifanyike kwa ajili ya kuwasaidia walemavu na wenye mahitaji maalum kitaifa, pale inapojulikana idadi yao kamili.







# Mkakati endelevu NGO kuzinduliwa Sep. 29

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MKAKATI wa kitaifa wa uendelevu wa mashirika yasiyo ya kiserikali (NGO), unatarajiwa kuzinduliwa Septemba 29 na 30, mwaka huu jijini Dodoma na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa.

Kaimu Katibu Mkuu Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Amon Mpanju, alisema hayo juzi alipokuwa akizungumza na wadau wa mashirika hayo kwenye kikao cha kupitia rasimu ya mkakati huo.

Alisema kikosi kazi kimekamilisha uchambuzi wa maoni yaliyopokewa na tayari kimeandaa rasimu ya Mkakati wa Kitaifa wa Uendelevu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NSNS).

"Ninayo furaha kwamba tunayo rasimu ambayo baada ya maoni ya leo (juzi) inafaa kutoa mwelekeo wa namna mashirika yasiyo ya kiserikali yanaweza kuwa endelevu hapa nchini.

"Ni matumaini yangu mtashiriki kwa ukamilifu katika kutoa maoni chanya yatakayosaidia kuboresha rasimu iliyoandaliwa na kikosi kazi na hatimaye kuwezesha utekelezaji wa mkakati huo kwa ajili ya uendelevu wa mashirika yasiyo ya kiserikali hapa nchini na mustakabali wa Maendeleo ya Jamii na Taifa kwa ujumla," alisisitiza Mpanju.

Aliwataka wadau kutoa maoni dhidi ya rasimu hiyo kwa ajili ya kupata mkakati ambao utakuwa tayari kuzinduliwa na kutekelezwa na mashirika hayo.

Akitoa taarifa ya kikosi kazi cha uratibu wa mkakati wa kitaifa wa uendelevu wa mashirika yasiyo ya kiserikali, Nesia Mahenge, alisema kikosi hiko kimefanikiwa kupokea maoni kutoka kwa wadau mbalimbali ndani ya Tanzania Bara na hivyo kufanikisha kupata rasimu hiyo muhimu kwa maendeleo ya NGO na taifa kwa ujumla.



Mkuu wa Mkoa wa Geita, Martin Shigela (kulia), akikabidhi vitabu kwa Mwanafunzi wa darasa la nne wa Shule ya Msingi Mkoani, Zuhura Athumani, vilivyotolewa na Shirika la Plan International kupitia mradi wao wa kuwawezesha wasichana kuendelea na masomo wa KAGIS, vyenye thamani ya zaidi ya sh. milioni 438 katika uwanja wa shule hiyo juzi. **PICHA: JOCTAN NGELLY**

# Machifu waombwa kuacha tabia ombaomba

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

MWENYEKITI wa Baraza la Machifu Mkoa wa Dodoma, Yasin Bilinje, amewaonya machifu wenzake kuacha tabia ya kupita katika ofisi za serikali kutumia vyeo vyao kuomba misaada.

Pia amewataka machifu hao kufanya kazi kwa kushirikiana na serikali na jamii katika kutatua kero ikiwamo kukemea maovu na ukatili wa kijinsia unaofanywa katika familia.

Bilinje alisema hayo jana alipokuwa akizungumza kwenye mkutano mkuu wa uchaguzi wa machifu uliofanyika jijini hapo.

Alisema moja ya majukumu ya machifu ni kuhakikisha wanafanya kazi kwa kushirikiana na serikali na jamii ili kutatua kero zinazowakabiri wananchi.

"Hivyo kazi ya machifu si kuzurura mitaani na ofisini bali wajibu wao ni kuhakikisha wanaisaidia serikali katika kutatua kero zinazotokea kwenye familia zikiwamo za ukatili na zile za kukeketa mtoto wa kike," alisema.

Hata hivyo, aliwataka machifu hao kufanya kazi zao kwa kufuata sheria na katiba ya baraza ili waweze kuheshimiwa na jamii wanayoiongoza na serikali yao.

Naye Katibu wa Baraza la Machifu Mkoa wa Dodoma, Jackson Ndahani, alisema nafasi ya uchifu ipo kisheria hivyo wanatakiwa kijithamini na kujitambua ili waweze kufanya kazi zao kwa kujiamini.

Ndahani aliwataka machifu pia kudumisha mila na desturi ambazo zitasaidia kudumisha uwoto wa asili ambao unasaidia kuleta mabadiliko ya kimaendeleo.

Naye Mlezi wa Machifu Mkoa wa Dodoma, Mohamed Keba, aliwataka kuangalia uwezekano wa kuibua miradi ili waondokane na utegemezi kiuchumi unaowakabili hivi sasa.

Alisema pamoja na kazi waliyo nayo ni kuongoza watu lakini wawe na maono ya kuibua miradi yenye tija ambayo itawaletea mafanikio ya kiuchumi kupitia nyadhifa zao.

Keba ambaye alikuwa msimamizi wa uchaguzi huo wa machifu, pia aliwataka kuvunja makundi waliyokuwanayo katika uchaguzi badala yake wawe kitu kimoja.

Katika uchaguzi huo waliochaguliwa kwa nafasi ya mwenyekiti ni Yasin Bilinje, makamu mwenyekiti Jackson Tupa, Katibu Jackson Ndahani na msaidizi wake Asher Kamwaya.

# Prof. Juma awafunda majaji Mahakama Kuu

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

JAJI Mkuu wa Tanzania, Prof. Ibrahim Juma, amewataka majaji 21 wa Mahakama Kuu walioapishwa hivi karibuni na Rais Samia Suluhu Hassan, kuepuka marafiki, wenza ambao wanaweza kuwashawishi kuvunja maadili.

Prof. Juma alisema hayo juzi jijini hapa wakati wa mafunzo elekezi yaliyotolewa kwa ajili ya kuwaimarisha kabla ya kwenda kutekeleza majukumu yao mapya ya ujaji katika maeneo mbalimbali nchini.

Alisema jaji ni kielelezo cha heshima, imani na kuaminiwa, hivyo baada ya kuapishwa wanapaswa kukumbuka na kuitekeleza imani ambayo Rais amewapa kwa niaba ya Watanzania.

"Naomba mwende kutenda kazi kwa kufuata sheria. Mkifanya hivyo mtakuwa mmetekeleza imani mlioapa kwa ufasaha," alisema.

Hata hivyo, alisema kuna baadhi ya wajumbe wa Baraza la Kutunga Sheria walipendekeza mamlaka ya jaji yajengewe vizuio vingi vya kikatiba ili wananchi wajilinde endapo jaji atakiuka kiapo chake.

"Kafanyeni vizuri ili mkadhirishe uwezo, maadili na nguzo za kuaminiwa ambazo mmekabidhiwa kama majaji wa Mahakama Kuu ya Tanzania," alisema Prof. Juma.

Alisema pia uwezo, juhudi na maarifa yao yatajenga imani na kuaminiwa kwenu kwa namna ambavyo watafanya uamuzi kwa haki ikiwamo kuzingatia katiba, sheria, kanuni, taratibu, miongozo, mila na desturi za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Kuhusu mafunzo elekezi, Jaji Mkuu alisema yalilenga kuwajengea msingi wa kuifahamu mahakama, kufahamu mwelekeo wa mhimili wa Mahakama ndani ya maudhui ya mwelekeo wa Tanzania na dunia inayoizunguka.

Alisema majaji wa Tanzania hawawezi kujificha kwenye majalada ya mashauri peke yake bila kuisoma na kuielewa jamii na kuongeza kuwa jaji mahiri hajikiti katika majalada yanayohitaji uamuzi wake pasipo kusoma maandiko kuhusu mwelekeo wa nchi yake na nchi nyingine.

Akizungumzia kuhusu suala la mitandao ya kijamii, Jaji Mkuu alisema katika zama hizi za teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA), maoni mengi kutoka kwa wananchi kuhusu mahakama pamoja na uamuzi wa mahakama hupitia katika mitandao ya intaneti na ile ya kijamii.

Alisema mwongozo umetambua kuwa matumizi ya mitandao ya kijamii yameongezeka kiasi cha kuwa sehemu muhimu ya maisha ya kijamii ya watu na jamii na imebadili namna taarifa za watu na jamii zinavyokusanywa, tawanywa na kusambazwa.

Jaji Mkuu aliwataka kila jaji ajisomee mwongozo huo wa hiari, ambao utawasaidia kutafakari kila mara unapotumia mitandao ya kijamii kama unavuka mipaka ya kimaadili.





## Tuzo za uandishi zasogezwa mbele

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

TAASISI isiyo ya kiserikali ya Tulia Trust ambayo inaandaa Tuzo za Umahiri wa Uandishi wa Habari Mkoa wa Mbeya, imetangaza kusogeza tarehe ya wanahabari kuwasilisha kazi zao kutoka Septemba Mosi mpaka Septemba 30, mwaka huu.

Ofisa Mawasiliano wa Taasisi hiyo, Joshua Mwakanolo, aliyasema hayo jana alipozungumza na waandishi wa habari ambapo alisema hatua ya awali ilikuwa ya wanahabari wanaotaka kushiriki tuzo hizo.

Alisema mchakato huo umeenda vizuri na kulikuwa na mwitikio mzuri kwa wanahabari kuchukua fomu lakini mwitikio wa urejeshaji umekuwa sio mzuri hali ambayo imewalazimu kusogeza muda wa kurejesha fomu hizo.

Mwakanolo aliwataka wanahabari waendelee kuwasilisha kazi zao ambazo zitashindanishwa kwenye tuzo hizo ambazo alisema zitatolewa Septemba 15, mwaka huu.

"Kazi hizi zitapokelewa zikiwa kwenye flashi kwa wale wa video na sauti au vipande vya magazeti kwa wale waandishi wa magazeti, kazi hizi zinapokelewa kwenye ofisi zetu mbalimbali," alisema Mwakanolo.

Alisema masharti ya kushiriki tuzo hizo yameainishwa kwenye fomu ambazo zinatolewa na taasisi hiyo na hivyo akawataka wanahabari kuendelea kuchangamkia.

Tuzo hizo, alisema zitakabidhiwa na Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, kwa kushirikiana na taasisi mbalimbali za kihabari na kwamba washindi watapewa zawadi mbalimbali.



Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Kanda ya Nyasa, wakishiriki mkutano mkuu wa uongozi wa kujadili mikakati ya kukijenga chama hicho, jijini Mbeya juzi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# CHADEMA yakiri CCM muziki mnene

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Kanda ya Nyasa, kimekiri kuwa ni vigumu kukiondoa Chama Cha Mapinduzi (CCM) madarakani kwa kupiga kelele bila kuwa na mikakati ya maana.

Mwenyekiti wa CHADEMA Kanda ya Nyasa, Mchungaji Peter Msigwa, aliyasema hayo juzi kwenye mkutano wa uongozi wa kanda uliofanyika juzi jijini hapo. Alisema CCM ina mikakati mikubwa ya kushinda uchaguzi, hivyo ni vigumu kuiondoa madarakani kirahisi.

Alisema CCM imekuwa madarakani kwa muda mrefu na imekuwa ikishinda kila uchaguzi mkuu huku vyama vya upinzani vikilalamika kuwa vinaibiwa kura jambo ambalo alisema halina tija kwa wananchi wa Tanzania.

Msigwa alisema kwa sasa viongozi wa CCM wanajipanga kushinda uchaguzi mkuu wa 2025 lakini vyama vya upinzani, ikiwamo CHADEMA, vimejaa migogoro ambayo haina maana yoyote.

Alisema wanachama wa vyama vya upinzani wanatumia nguvu kubwa kupambania madaraka na migogoro mingine ya kurushiana maneno wakati CCM wakipanga mikakati ya aina mbalimbali ya kuendelea kushika dola.

"Tusijidanganye kwamba tutaiondoa CCM madarakani kwa kupiga kelele. Lazima tuwe na mikakati mikubwa kuliko wao. Wao wanapotambaa sisi tutembee, wao wakitembea sisi tukimbie na wao wakikimbia sisi turuke," alisema.

"Wao sasa hivi wanajipanga kwa ajili ya uchaguzi wa 2025 na wanajipanga vizuri sana. Iwe kuiba, kupora au njia zingine ambazo zitawafanya waendelee kuwa madarakani, sisi tutaendelea kulalamika kwamba tunaibiwa kura," aliongeza Msigwa.

Alisema vyama vya upinzani vimekuwa vikipiga kelele kwa zaidi ya miaka 20 lakini bado havijawa na mikakati ya maana ya kuviwezesha kushinda dola.

Makamu Mwenyekiti Mstaafu wa Baraza za Vijana wa CHADEMA (BAVICHA), Patrick Ole Sosopi, alisema katika kipindi cha miaka sita iliyopita, chama hicho kilipitia katika wakati mgumu ambapo walikuwa hawana nafasi ya kukijenga chama hicho.

Alisema serikali ya awamu ya tano iliweka mazingira ambayo yalikuwa magumu kwao kufanya siasa kwa madai kuwa baadhi ya wanachama walikuwa wanatekwa na kupotezwa hali iliyorudisha nyuma mapambano ya chama hicho.

Alisema baadhi ya wanachama wa chama hicho waliokuwa na roho nyepesi waliamua kuhamia CCM ili kuepuka mazingira magumu yaliyokuwapo wakati huo.

"Tunatakiwa tujitowe sadaka ili kuikomboa Tanzania kutoka kwenye mikono ya hawa CCM ambao wameliongoza taifa kwa zaidi ya miaka 60 sasa na hakuna maendeleo ambayo wameleta," alisema Ole Sosopi.

Mmoja wa wajumbe wa chama hicho taifa, Selestina Simba, aliwaomba viongozi wa ngazi zote za chama hicho kushiriki kushughulikia matatizo ya wananchi kuanzia ngazi za chini badala ya kuendelea kushughulikia matatizo ya kitaifa pekee.

Alisema yako matatizo ambayo yanaweza kutatuliwa ngazi za chini lakini kutokana na baadhi ya viongozi kutotimiza majukumu yao wanasababisha matatizo hayo kuendelea kuwapo na kuwatesa wananchi wa kawaida.

Katika hatua nyingine, Msigwa aliwataka viongozi wa chama hicho kufanya kazi kwa bidi ili kukijenga chama hicho.

# Trafiki warushiwa lawama kuhusu ajali

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

BAADHI ya madereva wa mabasi yanayofanya safari kati ya Jiji la Mbeya na Wilaya ya Mbarali, wamewalalamikia askari wa usalama barabarani wanaosimamisha magari bila utaratibu kuwa ndio chanzo cha ajali.

Madereva hao waliyasema hayo wakati wa Mkutano na Mkuu wa Operesheni wa Jeshi la Polisi Mkoa wa Mbeya, Addi Issango, wakati wa mkutano wa kuhamasisha uwekaji wa viakisi mwanga kwenye vyombo vya moto.

Mmoja wa madereva hao, Godwin Mwambene, alisema wao wanaanzia safari zake katika Kituo cha Mabasi cha Nanenane na wamewekeana utaratibu wa kupanga foleni na kuondoka kwenye kituo hicho kwa kupishana dakika 10.

Alisema kinachotokea ni kwamba askari wa usalama barabarani wanawasimamisha maeneo mbalimbali na kuwakagua kwa muda mrefu hali ambayo inasababisha magari hayo kukutana kwenye baadhi ya vituo na kuanza kukimbizana.

Mwambene alisema askari hao wanaanza kusimamisha mabasi kwenye Kituo cha Nsalaga mpaka wanapofika Rujewa hali ambayo inasababisha mabasi hayo kukimbizana na kuwapunguzia umakini madereva.

Alisema kitendo cha maaskari kuwasimamisha mara kwa mara na kukagua magari kinawasababishia madereva hao kuendesha magari huku wakiwa na wasiwasi.

"Kinachotushangaza ni kwamba vituo vya kukagua magari viko vingi na viko jirani jirani mno. Tunajikuta wakati mwingine tumeongozana mabasi manne hali ambayo inatufanya tuwe tunakimbiza magari ili kuwahi abiria wa mbele," alisema Mwambene.

"Lakini sisi hatujavamia hii kazi, tumeenda darasani na hawahawa maaskari ndio walioupatia leseni za kuendesha magari, sasa huu ukaguzi unakuwa kama hawatuamini kabisa, tunaomba vituo hivi vipunguwe," aliongeza.

Mwambene alisisitiza kwamba hawapingi ukaguzi huo wa mabasi lakini wanachopinga ni vituo hivyo kuwa jirani jirani hali ambayo inawasababishia kuendesha mabasi kwa kasi ili kukimbiana na kuwahi abiria.

Alisema mbali na askari hao wanaokagua magari pia wako wanaotumia tochi za kuangalia mwendokasi na kwamba wakati mwingine huwa wanasimamisha mabasi bila utaratibu na hawajaandaa mazingira mazuri ya maeneo ya kukagua magari. Naye Masigwa Mayori ambaye ni dereva wa trekta, alisema maaskari wamekuwa wakiwafukuzia mpaka kwenye mashamba hali ambayo huwa inawasababishia ajali ambazo zinahatarisha maisha yao.

Alisema wakati mwingine maaskari hao wa usalama barabarani wamekuwa wakiwafukuzia hata nyakati za usiku hali ambayo huwa ni hatari zaidi.

Mayori alisema utaratibu huo ni mbaya na unasababishia madereva kuumia na wakati mwingine kuharibika vyombo vyao.

"Elimu tunayopewa hapa ni nzuri sana lakini tunachoomba ni kwamba maaskari waache kutukimbiza usiku, wanatusababishia matatizo makubwa sana," alisema Mayori.

Akijibu malalamiko hayo, Issango alisema wataendelea kulishughulikia jambo hilo ili kumaliza matatizo hayo ya madereva.

Alisema lengo la Jeshi la Polisi ni kuhakikisha linamaliza ajali zinazokuwa zinatokea mara kwa mara na kugharimu maisha ya watu na mali zao.

Kwa sasa, alisema wanahamasisha madereva na wamiliki wa magari kuweka viakisi mwanga kwenye magari na vyombo vingine vya moto ili kupunguza ajali ambazo zimekuwa zikitokea nyakati za usiku.





# Mwinyi azipongeza taasisi uimarishaji huduma za jamii

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi amesema ushiriki wa taasisi zisizo za kiserikali katika uimarishaji wa huduma za kijamii ni muhimu kwa kuzingatia serikali haina uwezo wa kuwafikia wananchi wote.

Dk. Mwinyi aliyasema hayo Ikulu Zanzibar, alipozungumza na viongozi wa Taasisi za Milele Zanzibar Foundation na IFRAJ waliofika kumsalimia pamoja na kuelezea shughuli mbalimbali zinazofanywa na taasisi hizo.

Alisema kwa kipindi kirefu sasa taasisi hizo zikifanya kazi kubwa ya kuisaidia serikali, hususan katika uimarishaji wa sekta za huduma ya jamii.

Alizipongeza taasisi hizo kwa kufanya kazi kubwa na kuwa taasisi zinazofanya vyema zaidi hapa nchini katika kuisaidia serikali uimarishaji wa sekta za huduma za jamii, ikiwamo afya, elimu, maji na uwezeshaji wajasiriamali.

"Ninaridhika na kazi kubwa mnayofanya kwa kuwa inagusa vipaumbele vya serikali katika kuimarisha huduma za jamii," alisema.

Alifurahishwa na kazi kubwa inayofanywa na taasisi hizo katika kujenga mifumo pamoja na kuzingatia umuhimu wa ujenzi wa miundombinu, uwepo wa rasilimali watu na mahitaji ya vifaa katika sekta hizo.

Dk. Mwinyi alisema Zanzibar inakabiliwa na tatizo kubwa la ukosefu wa majisafi na salama na hatua inayochukuliwa na taasisi hizo ya kusaidia upatikanaji wa pampu pamoja na uchimbaji wa visima ni ya kupongezwa.

Naye Mkuu wa Miradi wa Taasisi ya Milele Zanzibar Foundation, Khadija Ahmeid Sharrif, alisema taasisi hiyo ipo mstari wa mbele kuisaidia jamii kupitia sekta mbalimbali.

Kwa upande wake, Meneja wa Taasisi ya IFRAJ, Abdalla Said Abdalla, alisema taasisi hiyo inajishughulisha na ujenzi wa nyumba za makazi kwa wananachi wenye kipato cha chini na sasa wanakamilisha ujenzi wa nyumba 500 zinazogharimu zaidi ya Sh. bilioni 7.5.

# Mtoto aliyeokolewa kwenye moto na bibi aendelea vizuri

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

NADIL Issa (5) ambaye amenusurika kifo baada ya bibi yake kuruka naye kutoka ghorofani kutokana na nyumba yao kuungua moto, anaendelea vyema na matibabu.

Bibi wa mtoto huyo Rehema Chande (70), alipoteza maisha eneo la Mkunazini Mjimkongwe Zanzibar, baada ya kuanguka kutoka ghorofani akijiokoa yeye na mjukuu wake baada ya nyumba yao kuungua.

Akizungumza na Nipashe jana, Ofisa Muuguzi katika wodi ya watoto hospitalini hapo, Thuwaiba Said, alisema hali ya mtoto huyo inaendelea vizuri na hakupata majeraha makubwa. Muuguzi huyo alisema, mtoto huyo alifikishwa hospitali hapo juzi majira ya saa saba mchana na kuanza kupatiwa matibabu.

"Mtoto tulimpokea majira ya saa saba mchana Jumanne kutokana na majeraha aliyoyapata baada ya bibi yake kujirusha ghorofani akijiokoa na moto uliozuka katika nyumba wanayoishi," alisema.

Alisema mtoto amefanyiwa vipimo vyote hakukutwa na majeraha makubwa kutokana na kuangukia kifuani kwa bibi yake.

Mama wa mtoto huyo, Hawa Kundi Haji, alisema alipigiwa simu na majirani wa mkwe wake (marehemu) kuwa amefariki dunia na mtoto wake amepelekwa hospitali.

"Baada ya kupata taarifa nilipatwa na mshtuko mkubwa na kulazimika kukimbilia hospitali, hata hivyo nashukuru kukuta hali ya mtoto wangu sio mbaya ingawa nina majonzi ya kumpoteza bibi yake ambae ndiye alikuwa mlezi wake," alisema.

Alisema mtoto wake alikuwa akiishi na bibi na baba yake ambaye waliachana na kila mmoja kuishi eneo lake.

Baba wa mtoto huyo, Issa Ramadhan Ismail, alisema wakati tukio la moto linatokea hakuwapo nyumbani na alipokea taarifa kwa mshtuko mkubwa. Aliiomba serikali na watu mbalimbali kumsaidia kwa sababu hakuna kitu kilichookolewa katika nyumba yao baada ya kuteketea kwa moto.

"Tukio hili sitaweza lisahau maishani mwangu, kwanza nimepoteza mama yangu mzazi, mtoto wangu amepata majeraha na hapa unapotuona hatuna hata nguo ya kuvaa zaidi ya hizi tulizovaa mwilini kwa sababu hakuna kitu kilitoka ndani ya nyumba vyote vimeungua," alisema kwa masikitiko.

Alisema baada ya ndoa yake kuvunjika, mtoto wake Nadil akiwa na umri wa miaka miwili, alilelewa na bibi yake kumpunguzia mzigo wa malezi mtalaka wake.

Alisema ingawa walikuwa wakiishi pamoja na mama yake, lakini muda mwingi mtoto alikuwa na bibi yake na huko hospitali anamtaja bibi yake mara kwa mara.

**WAZIRI AZUNGUMZA**

Akizungumza baada ya kumkagua mtoto Hospitali, Waziri wa Jinsia, Wazee na Watoto, Riziki Pembe, alisema Rehema (marehemu) anahitaji kupewa nishani ya ushujaa kwa kumuokoa mtoto huyo katika tukio la ajali ya moto.

"Kwa kweli tukio hili ni la kusikitisha, lakini bi Rehema licha ya kufariki dunia ni shujaa kwa kujitoa muhanga kwa kumuokoa mjukuu wake...ndiyo wazazi tunavyokua hasa mzazi wa kike," alisema.

Alisema wanawake ndiyo walezi wakuu wa watoto na wapo tayari kujitoa muhanga ili kunusuru maisha ya watoto kama kitendo alichokifanya bi Rehema.

Alitoa pole kwa familia hiyo kwa kuondokewa na mpendwa wao na kuwataka kuwa na subira katika kipindi hiki kigumu cha msiba huo.



Waziri wa Jinsia, Wazee na Watoto Zanzibar, Riziki Pembe, akimjulia hali mtoto, Nadil Issa, aliyenusurika kifo baada ya bibi yake kuruka naye kutoka gorofani wakati akijihami dhidi ya moto kwenye nyumba wanayoishi eneo la Mji Mkongwe, akiwa anaendelea kupatiwa matibabu katika Hospitali ya Mnazi Mmoja Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Kampuni za teknolojia zaanza uwekezaji Z'bar

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imezindua mpango wa kuvutia na kukaribisha kampuni za teknolojia visiwani humo huku kampuni ya Masoko inayokua kwa kasi barani Afrika ikifungua ofisi ya kwanza Zanzibar.

Akizungumza baada ya uzinduzi wa mpango huo wa kituo cha biashara cha Pavillion katika Mji wa Fumba, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi Uchumi na Uwekezaji Mudrik Ramadhan Soraga, alisema utekelezaji wa mpango huo utasaidia kukuza matumizi ya teknolojia na kukuza uchumi wa taifa na ajira kwa vijana.

Waziri Soraga alisema,kampuni za teknolojia hazitahitaji tena kufungua ofisi na kuhamisha watu wao kwenda Dubai au London kusimamia shughuli zao barani Afrika.

"Tunatoa mazingira ya wazi na wezeshi kwa makampuni yote ya teknolojia na washiriki wa timu zao kuwa mjini Zanzibar mojawapo ya maeneo yanayovutia zaidi duniani kuruhusu kila mtu anayefanya teknolojia kwa ajili ya Afrika kuwa na msingi barani humu," alisema.

Alisema kampuni ya Silicon Zanzibar inaunga mkono sera ya serikali ya Uchumi wa Buluu ili kukuza maendeleo ya kiuchumi kwa kupitia chini ya mazingira na mahitaji ya rasilimali endelevu.

Alisema wafanyabiashara wa kiteknolojia wana uwezo wa kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi hasa kiuchumi kwa vile hawategemei hali ya hewa, jambo ambalo litaisaidia Zanzibar kuinua uchumi wake dhidi ya sekta za msimu kama kilimo na utalii.

Alisema tukio hilo ni la kihistoria kwa Zanzibar na ndiyo kituo cha kwanza baada ya kuweka mkakati wa kuanzisha mpango maalum wa kualika kampuni za teknolojia kutoka nchi mbalimbali duniani kuwekeza visiwani humo.

Aidha, alisema lengo la mpango huo ni kuruhusu shughuli za uwekezaji kuendelea kuchukua nafasi kwa kukaribisha kampuni mbalimbali kutoa huduma ikiwamo za vyakula na matumizi mengine ya nyumbani kwa wakazi wa eneo hilo ili kupatikana kwa karibu zaidi. Waziri Soraga alisema uwekezaji katika teknolojia unakwenda sambamba na sera ya serikali ya uchumi wa buluu na kila sekta inayoguswa ni suala la mifumo ili kuvutia wawekezaji.

Hata hivyo, alisema mtazamo wa serikali kwa sasa ni uwekezaji katika nyanja zote na kwamba ni vyema kuangalia zaidi fursa zilizo katika eneo hilo ikiwamo za sekta ya uchumi wa buluu katika kutumia rasilimali zilizomo kwa kuzingatia uchumi endelevu.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni ya uhandisi ya CPS, Sebastian Dietzold, alisema CPS inasaidia kuendeleza jumuiya zenye nguvu zinazoongeza thamani kwa wawekezaji kama Wasoko, kwa madhumuni ya msingi ya kuwawezesha watu wa Zanzibar na wafanyabiashara.

"Silicon Zanzibar tayari imevutiwa na kampuni ya Wasoko kama mshirika wake wa kwanza, ni kampuni inayokua kwa kasi barani Afrika kama inavyotambuliwa na Financial Times, imetangaza kufungua kituo kipya katika Mji wa Fumba sambamba na kuwatumia zaidi ya wafanyakazi 40 wa teknolojia na viongozi wakuu akiwamo Mkurugenzi Mtendaji wa Wasoko, Daniel Yu," alisema Sebastian. Alisema kampuni yao inaongeza thamani kwa jumuiya za wawekezaji wa ndani na nje na imani yake kwamba kituo hicho kitaongeza uwekezaji na thamani ya mji huo wa kisasa.

Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Vitega Uchumi Zanzibar (ZIPA), Sharif Ali Sharif, aliahidi kwamba ZIPA itaendelea kutoa ushirikiano ili lengo la kuanzishwa mradi huo linatimia kwa sababu wawekezaji hao wanaisaidia serikali katika kuinua uchumi wa nchi.

Aliwapongeza wawekezaji hao kwa kutumia teknolojia ya kusambaza bidhaa madukani ikiwamo vyakula kwa sababu wakazi zaidi ya 500 wanaokaa katika mji huo watapata fursa ya teknolojia hiyo kwa kupatiwa bidhaa wanazozitaka.

Eneo la uwekezaji Fumba town limeshajengwa nyumba 234 na lina zaidi ya wakazi 500 hadi sasa, mpango wa Zanzibar Silicon utaruhusu uwekaji wa maduka na huduma muhimu.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## ANATAFUTWA



Ndugu **SHAMTE MOHAMED** anatafutwa na polisi kwa tuhuma za kujihusisha na vitendo vya kinyume na maadili na Wizi wa kuaminiwa, Taarifa imeripotiwa polisi **No. UBUNG/RB/174/22** Yeyote mwenye taarifa zake anaombwa atoe taarifa polisi kituo cha karibu naye

## ANATAFUTWA



Ndugu **Fadhili Juma Ngongota** anatafutwa na polisi kwa tuhuma za kujihusisha na vitendo vya kinyume na maadili na Wizi wa kuaminiwa, Taarifa imeripotiwa polisi **No. DAR/RB/3520/22** Yeyote mwenye taarifa zake anaombwa atoe taarifa polisi kituo cha karibu naye **au Piga simu no 0789 133141**

## KUPOTEA KWA PASSPORT



**STEPHAN JOHN MABULA** Mtajwa hapo juu anatangaza kupotelewa na Hati yake ya kusafiria (Passport) yenye namba **TAE 390058** Kwa atakaeiona atoe taarifa Kituo chochote cha polisi kilichopo karibu kwa KUMB: **KAG/KYA/187397/2022.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO**
**WILAYA YA MJINI MOROGORO**

**KITUO CHA MJINI MKOA WA MOROGORO**

**Usimamizi wa Mirathi Na......50/2022**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU: CAROLINA IVO WA UALIMU**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA USIMAMIZI WA MIRATHI YALIYOLETWA NA GEORGE EXVERY CLEMENSI**

**TANGAZO**
**(kanuni ya 5(2)ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tahehe 08 Mwezi 09 Mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Zingatia;
- Wosia wa marehemu huyo upo mahakaman na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia wowote.

Imetolewa leo tarehe 01mwezi 09 mwaka 2022

**HAKIMU MFAWIDHI**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**ANNASTAZIA CONSTANTINE MANUMBU**

Anatangaza kupotelewa kwa kadi ya pikipiki yenye namba za usajili **MC 703 CVW** yeyote atakae iona atoe taarifa kituo cha polisi au piga simu namba **0739552556**

**DSM /PHQ/RB/346907/2022**

## KUPOTEA KWA KADI YA TOYO MOTORCYCLE

**ALLI KONDO MBWANA**

Anatangaza kupotelewa kwa kadi ya toyo motorcycle yenye namba za usajili **T 825 CSE** yeyote atakae iona atoe taarifa kituo cha polisi au piga simu namba 0716999926.

**MOR /MOR/RB/323290/2022.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO**

**WILAYA YA MJINI MOROGORO**

**KITUO CHA MJINI**
**MKOA WA MOROGORO**

**Usimamizi wa Mirathi Na......57/2022**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU: RAHMA AHMED IBRAHIMU WA JUWATA**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA USIMAMIZI WA MIRATHI YALIYOLETWA NA FARIDA AHMED IBRAHIMU**

**TANGAZO**
**(kanuni ya 5(2)ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tahehe 09 Mwezi 09 Mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Zingatia;**
- Wosia wa marehemu huyo upo mahakaman na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia wowote.

Imetolewa leo tarehe 25 mwezi 08 mwaka 2022

***HAKIMU MFAWIDHI***

**KUITWA SHAURINI**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA (MCA/63)**

**Katika Mahakama ya Mwanzo Muleba Mjini**

**Wilaya ya Muleba**

**Talaka madai no 11/2022**
**JAMHURI**

**Kwa Magreth Yunusu Nkolo**
**WA Izigo – Kaboya**
**K.K**
**Afisa Mtendaji**
**Kata Izigo**

Unaamrishwa na Jamhuri Uhudhurie mbele ya Mahakama hii siku ya IJUMAA Tarehe 9/9/2022 asubuhi kuwa mdaiwa katika shauri lililoko mbele ya Mahakama hii ukifika usiondoke bila ya ruhusa ya mahakama na unaonywa kwamba usipuuzie wito huu.
Ukipuuzia wito huu bila udhuru wa maana hati itatolewa kukulazimisha kuhudhuria.
Hati hii inatolewa kwa amri yangu na muhuri wa mahakama hii leo tarehe 4/08/2022
Kuitwa shaurini hii kwa maombi ya :-
Mpoki Nicodemu Kalulunga wa Kaboya

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 121 OF 2022**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE GREYSON SAMWEL KITAJA Of Ipagala East within Dodoma City**
**And**

**IN THE MATTER OF APPLICATIONFOR LETTERS OF ADMINISTRATION**

**BY OSPHIA KAMLI ISANZU**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules Gn.369 Of 1963)**

ALL PERSONS Claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Admiration is made to the above named petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the **13st Day of 09, 2022.**

**Dated at Dodoma this 29th day of AUGUST, 2022**

RESIDENT MAGISTRATE

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**APOLINARY MARIA D'COSTA**

anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **MITSUBISHI PAJERO** yenye namba za usajili **T705 AGU,** chasis namba **conv460sj00179,** yeyote atakayeiokota atoe tarifa kituo chochote cha polisi.
Polisi taarifa **ARU/ARU/RB/347227/2022**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya DODOMA MJINI**

**Kituo cha CHAMWINO MJINI Mkoa DODOMA**

**Usimamizi wa mirathi Na. 45/2022**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU ABDALLAH O. JUMA wa Chang'ombe**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA OMARY ABDALLAH JUMA**

**TANGAZO**

**(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 12 Mwezi 09 Mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
Imetolewa leo Tarehe 26 Mwezi 08 Mwaka 2022

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**LUCY ESAU MBEDE**

anatangaza kupotelewa na kadi ya GARI (SUZUKI-CARRY) yenye namba za usajili **T 240 DFQ.** Chasis Namba: **DD51T396105.** Kadi Namba: **8097706.** Engine Namba: **F6AEAE6105.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi RB namba **MKB/RB/150/2022.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika mahakama ya mwanzo ya wilaya TEMEKE**

**Kituo JUMUISHI mkoa DAR ES SALAAM**

**Usimamizi wa mirathi na 1639/2022**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU SHABANI MOHAMED MZIWANDA**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA FATUMA MZIWANDA MOHAMEDI**

**TANGAZO**

**(kanuni ya 5(2) ya kanuni za usimamizi wa mirathi mahakama za mwanzo)**


Watu wote wanodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 21 mwezi 09 mwaka 2022 kabla ya huyo muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi.

**Zingatia.**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa marehemu anaweza kuuleta mahakama kukaguliwa.

**Imetolewa leo tarehe 31 mwezi 08 mwaka 2022.**

HAKIMU


***Uza,***
***Chenye Thamani Kubwa***
***Kwa Kutangaza Nasi***
***Kwa Bei Poa***
***Tupigie 0782253676***


TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Kesi pingamizi urais Kenya yapamba moto

**NAIROBI, KENYA**

MAHAKAMA ya Juu nchini Kenya imeelezea kuwa mchakato wa kuingia kwenye mfumo wa mtandao wa teknolojia wa Tume ya Uchaguzi na Mipaka (IEBC) umekamilika.

Kwa mujibu wa taarifa iliyochapishwa jana na DW, Jaji Isaac Lenaola wa jopo la majaji saba aliielezea Mahakama ya Juu kuwa walipokea ripoti kamili ya kikosi cha ufundi na kwamba kila agizo limefuatwa.

Wakili wa mgombea wa urais wa Azimio la Umoja One Kenya, Raila Odinga, alilalamika kuwa hawajapata fursa ya kuingia kwenye seva zote nane za tume ya uchaguzi na kwamba kwenye hiyo moja waliofanikiwa kuiona, maelezo yalikuwa yamefutwa.

Wakili Phillip Murgor, alilalamika mbele ya mahakama kwamba IEBC ilikataa kuheshimu agizo la mahakama kwa kuwanyima maofisa wake fursa ya kuingia na kufanya uchunguzi katika seva zote nane.

"IEBC ilikataa seva zake kuchunguzwa, walituruhusu kuchunguza seva tano pekee na tukaona kiwango kikubwa cha ufutaji wa data muhimu na kwasababu muda unayoyoma watatupatia habari zisizo muhimu," alisema Murgor.



Mawakili James Orengo, Paul Mwangi, Philip Murgor na Julie Soweto wakiwasilisha hoja zao katika mahakama ya juu dhidi ya pingamizi la kura za uchaguzi wa urais nchini Kenya. **PICHA: MTANDAO**

### IEBC ILITIMIZA WAJIBU KIKATIBA

Mawakili wanaoiwakilisha tume huru ya uchaguzi nchini Kenya IEBC, walimtetea mwenyekiti wake anayeandamwa na madai ya kufanya kazi bila ushirikiano na kuwatenga makamishna wanne.

Akiwa mbele ya jopo la majaji saba wa Mahakama ya Juu, mwanasheria mkuu wa zamani wa Kenya, Profesa Githu Muigai, alieleza kuwa mwenyekiti wa tume hiyo, Wafula Chebukati, ni shujaa na alitimiza wajibu wake kama ilivyomwagiza katiba.

Profesa Githu pia alisisitiza kuwa IEBC ilifuata maelekezo ya Mahakama ya Juu yaliyotolewa mwaka 2017 wakati ambapo uchaguzi mkuu ulifutiliwa mbali ushindi wa Rais Uhuru Kenyatta na kwamba haikurudia makosa ya wakati huo.

Mwanasheria mkuu huyo wa zamani aliweka bayana kuwa uchaguzi ulikuwa na makosa hapa na pale ila hakuna sababu ya msingi ya kufutilia mbali matokeo yake kwa kuwa hakuna ushahidi.

### B.V YAKATAA KUFUNGUA SEVA

Kwa mujibu wa BBC, kampuni iliyotoa teknolojia ya kupigia kura kwa tume ya uchaguzi ya IEBC nchini Kenya Smartmatic International Holding (B.V) ilikataa kufungua seva za kituo kikuu cha kitaifa cha kuhesabia kura kutokana na masuala ya usalama.

Katika barua iliyoziandikia pande husika za kesi ya kupinga uchaguzi inayoendelea katika mahakama ya juu, kampuni hiyo ilisema kwamba ufunguzi wa mfumo huo uliotumika kupeperusha matokeo ya fomu 34C utakiuka haki zake za kimsingi.

Pia inaelezwa kuwa barua hiyo ilikuja baada ya tofauti iliyoibuka kati ya walalamishi wanaopinga uchaguzi wa urais na tume ya uchaguzi IEBC kuhusu kuingia katika seva hizo ili kuchunguza kilichopo ndani yake.

### KURA 4,463 ZILITOLEWA

Kwa mujibu wa BBC, wakili katika timu ya wanasheria wa kiongozi wa Azimio Raila Odinga Julie Soweto, alidai kuwa kura 4,463 zilitolewa kutoka kwa mteja wake na kuongezwa kwa Rais mteule William Ruto katika Kaunti za Bomet, Kiambu, Kakamega, Nairobi na Baringo.

Julie alilalamika kwamba kulikuwa na tofauti katika fomu 41 za 34A kutoka Bomet, Kiambu na Kakamega zilizopewa maajenti na zile zilizopo kwenye tovuti ya Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka (IEBC), ambazo ziliwasilishwa katika kituo cha kitaifa cha kujumlisha kura cha Bomas.

"IEBC ilinunua seti mbili za fomu 34A licha ya kutakiwa kununua kijitabu kimoja pekee ambacho kingetumiwa katika vituo vya kupigia kura huku 2/2 kikihifadhiwa kwenye bahasha isiyoweza kuguswa, hati ya kiapo ya Celestine Anyango inaonyesha ubaya wa kimakusudi katika matumizi ya fomu.

"Fomu ambazo mawakala wanazo na fomu kwenye tovuti ni sawa katika vipengele vyote namba za mfululizo, mihuri na sahihi, hata hivyo, takwimu katika fomu zimebadilishwa na ni tofauti," alisema.

Wakili Mkuu James Orengo, ambaye yupo katika timu ya wanasheria wa Odinga, alidai kuwa IEBC haina utendakazi na haiwezi kufanya uchaguzi, huku akidai kuwa fomu hizo zilibadilishwa.

### KURA KUHESABIWA UPYA

Katika hatua nyingine Mahakama ya Juu iliiamuru tume ya uchaguzi IEBC, kuwasilisha Fomu 32As na Fomu 34 kutoka vituo 41 kama ilivyoelekezwa siku ya Jumanne.

Msajili wa mahakama aliifahamisha mahakama ya juu kwamba wahusika mbalimbali hawakuweza kukubaliana jinsi ya kuendesha zoezi hilo kutokana na agizo lililotolewa kuhusu uchunguzi na kuhesabiwa kura upya Agosti 30, mwaka huu.

Pia ilielezwa kuwa mawakili wa kampuni ya (Otieno Ogola & Company Advocates) waliiandikia mahakamu ya juu wakisema wanataka fomu 32 A kutoka vituo vyote 229, nao mawakili wa Njoki Mboshe waliiandikia mahakama hiyo wakitaka fomu za vituo 238 huku walalamishi nao wakiomba vituo 517, na kwamba kutokana na muda agizo hilo halitafanikiwa.

"Tunaamuru kwamba IEBC itoe Fomu 32 na 34 A Kitabu mbili kutoka kwa vituo 41 katika maombi ya Celestine Anyango Apiyo, hiyo ndiyo njia pekee ambayo zoezi hilo linaweza kuwa na maana," alisema Jaji Lenaola.

Aliongeza kuwa kwenda zaidi ya vituo vilivyowekwa kutaunda kesi mpya kutokana na muda mfupi uliotolewa wa uchunguzi huo.

### MAMBO 9 YATAKAYOZINGATIWA

Aidha, mahakama hiyo ya juu ilisema itazingatia masuala tisa katika usikilizwaji wa kesi hiyo kabla ya uamuzi wake unaotarajiwa kutolewa Septemba 5, mwaka huu.

Majaji saba walinuia kutathmini iwapo teknolojia ya uchaguzi, iliyotumiwa hasa kufuatilia matokeo kutoka vituo vya kupigia kura hadi kituo cha kitaifa cha kuhesabia kura, ilikidhi viwango vya uadilifu, uthibitisho, usalama na uwazi.

Vile vile ilibainishwa kuwa makosa katika mfumo wa kielektroniki yalisababisha Mahakama ya Juu kufutilia mbali uchaguzi uliopita wa urais wa Agosti 2017 ambao ni wa kwanza barani Afrika, baada ya Odinga kukata rufani.

Agosti 30 mahakama hiyo iliamuru IEBC kumpa Odinga na walalamishi wengine idhini kamili na usiozuiliwa kutazama seva za kompyuta zilizotumiwa kwa uchaguzi, huku Odinga akidai kwamba wavamizi walivamia seva na kuzipakia fomu za matokeo ya uchaguzi ya uongo, madai ambayo rais wa IEBC alikanusha.

Pia alisema kuwa matokeo katika angalau vituo 14 kati ya 46,000 yanapaswa kupitiwa na kuhesabiwa upya. "Baada ya kutathmini uwazi wa kura hiyo, itabainisha iwapo William Ruto amefikia kiwango cha kikatiba cha asilimia 50 pamoja na kura moja kutangazwa kuchaguliwa katika duru ya kwanza," alisema.

Kwa mujibu wa RFI, tangu mwaka 2002, chaguzi zote za urais nchini Kenya zimekuwa zikipingwa, wakati mwingine kusababisha ghasia za baada ya uchaguzi na machafuko hasa ya mwaka 2007.

Wakati wa kampeni za uchaguzi, Ruto na Odinga walikuwa wameahidi kutatua tofauti zozote mahakamani badala ya mitaani.

Ikiwa Mahakama ya Juu itabatilisha uchaguzi huo, ni lazima kura mpya ifanyike ndani ya siku 60, na kwamba iwapo itathibitisha matokeo hayo, William Ruto atakuwa rais wa tano wa Kenya tangu nchi hiyo kupata uhuru mwaka 1963.

# KMKM YAENDELEZA UBABE, LIGI KUU Z'BAR IKIANZA LEO

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

WAKATI Ligi Kuu Zanzibar msimu wa 2022/2023 inaanza leo kwa Malindi kuivaa Black Sailor kwenye Uwanja wa Amaan, KMKM imetwaa Ngao ya Jamii baada ya kuifunga Kipanga bao 1-0, hapo juzi jioni.

Kocha wa Black Sailor, Saleh Machupa, alisema mchezo huo utakuwa mgumu lakini timu yake imejipanga kutopoteza pointi katika mechi hiyo ya kwanza ya msimu huu.

"Nawafahamu Malindi, inawachezaji wazuri na wenye uzoefu lakini hii ni ligi na michezo ya mwanzo katika ligi kuu huwa haitabiriki, lolote linaweza kutokea," alisema Machupa.

Naye Kocha Msaidizi wa Malindi, Ali Kisaka, alisema wamejipanga imara kuhakikisha wanaanza vyema msimu huu wa ligi kwa kuvuna pointi zote tatu muhimu.

"Katika mchezo huu kila timu inahitaji kufanya vizuri na kupata alama tatu, lakini tunajua michezo ya ligi inavyokuwa migumu hususani ya mwanzoni, kila mchezaji anakuwa na hamu ya kuifanyia makubwa timu yake, tunajipanga kupata alama tatu," alisema Kisaka.

Ligi hiyo itaendelea tena kesho kwa Kipanga kuikaribisha Zimamoto wakati KMKM itawaalika Kundemba kwenye Uwanja wa Amaan kuanzia saa 1:00 usiku.

Wakati huo huo, KMKM imetwaa Ngao ya Jamii baada ya kuifunga Kipanga bao 1-0 katika mchezo huo wa ufunguzi wa msimu mpya uliochezwa juzi jioni.

Bao pekee katika mechi hiyo lilipachikwa na Salum Akida dakika 90.

Kocha Msaidizi wa KMKM, Ame Msimu, alisema lengo la kwanza la kunyakuwa ngao limetimia na sasa ataendelea kujiimarisha ili kutetea ubingwa wa Ligi Kuu Zanzibar wanaoushikilia.

Msimu alisema anataka pia kuiona KMKM inajiimarisha na kufanya vizuri katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika itakayoanza hivi karibuni.

Kocha Msaidizi wa Kipanga, Khamis Hassan, aliliambia gazeti hili kupoteza mchezo wa Ngao ya Jamii haina maana wamepoteza matumaini ya kupambana kuwania taji la Ligi Kuu Zanzibar.

Kocha huyo alisema anaendelea kuijenga timu yake ili ipeperushe vyema bendera ya Zanzibar katika michuano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika.



Mchezaji wa All Stars Veterans, Rafiki Ntoke (kushoto), akijiandaa kumtoka nyota wa Mafather Veterans katika mechi ya kirafiki iliyochezwa kwenye Uwanja wa Jakaya Kikwete Youth Park jijini Dar es Salaam Jumapili iliyopita. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Makocha waitwa darasani Z'bar

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

SHIRIKISHO la Mpira wa Miguu Zanzibar (ZFF) linatarajia kuendesha mafunzo ya sheria 17 za mchezo huo kwa makocha wanaofundisha timu za Ligi Kuu visiwani hapa pamoja na wale wa Ligi za Kanda, imefahamika.

Mafunzo hayo yatakayofanyika leo na kesho, pia yatawahusisha manahodha wa timu zote zinazoshiriki ligi hizo.

Mkurungenzi wa Ufundi wa ZFF, Salum Ali Haji, aliliambia gazeti hili mafunzo hayo yataendeshwa na Mkufunzi wa ndani wa waamuzi, Ramadhani Ibada Kibo, na lengo lake ni kuwafahamisha kuhusu sheria zilizofanyiwa mabadiliko katika msimu huu wa 2022/2023.

Haji alisema, wanaamini mafunzo hayo yatawajengea makocha na manahodha hao uelewa mpana wa sheria za soka na hatimaye kusaidia kupokea maamuzi mbalimbali yatakayofanyika kwenye mechi wanazocheza.

"Makocha na wachezaji wamekuwa vinara wa kuwalalamikia waamuzi pale wanapofanya uamuzi wao, pengine hufanya hivi kwa kutokujua mabadiliko ya sheria au kufanya makusudi, naamini mafunzo haya yatawafungua na kumaliza malalamiko," Haji alisema.

Aliongeza kwa kuwataka washiriki kuzingatia elimu watakayopewa kwa kuyafikisha kwa timu wanazotoka ili kuleta ufanisi na mabadiliko katika kazi zao huku pia ikisaidia kumaliza dhana ya kuonewa.

## JKT Tanzania FC yaiwaza Ligi Kuu

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa JKT Tanzania umesema umejipanga kuhakikisha timu yao inarejea katika Ligi Kuu Bara msimu ujao na hilo ndio lengo kuu la kumwajiri kocha, Malale Hamsini.

Katibu Mkuu wa JKT Tanzania, Abdul Nyumba, alisema wamesajili kikosi imara kitakachosaidia kutimiza malengo yao katika Ligi ya Championship wanayoshiriki ambayo msimu mpya wa 2022/2023 utaanza ifikapo Septemba 17, mwaka huu.

Nyumba alisema wanaamini maboresho yaliyofanyika katika benchi la ufundi yatawasaidia kufikia malengo ya kurejea katika Ligi Kuu Tanzania Bara baada ya kufahamu walipokosea msimu uliopita.

Aliwataja wachezaji wapya 10 ambao wamewasajili kuongeza nguvu ni Hassan Kapalata, Emmanuel Kichiba, Ally Yusuph, Riphat Msuya, Mohammed Katoto, Maka Edward, Maulid Juma, Richard Jovit, Siraji Juma na Himid Yusuph.

"Msimu huu tumejipanga kurejea rasmi katika Ligi Kuu moja kwa moja, tumefanya usajili mzuri na kufanya Pre Season safi, hatutaki kucheza Play Off," alisema Nyumba.

Katika kujiandaa na msimu mpya, JKT Tanzania inatarajia kucheza mechi ya kirafiki dhidi ya Namungo FC leo kwenye Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam.

## Mieleka kufanya uchaguzi Oktoba

**Na Saada Akida**

UCHAGUZI Mkuu wa Chama cha Mieleka ya Ridhaa Tanzania (TAWF), umepangwa kufanyika ifikapo Oktoba 28, mwaka huu jijini Dar es Salaam.

Akizungumza jijini jana, Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano wa Baraza la Michezo la Taifa (BMT), Najaha Bakari, alisema fomu kwa ajili ya wadau wanaotaka kuwania nafasi mbalimbali zilianza kutolewa jana na mwisho wa zoezi hilo ni Oktoba 24, mwaka huu.

Bakari, alizitaja nafasi zinazowaniwa ni pamoja na Rais, Makamu Rais, Katibu Mkuu, Katibu Msaidizi, Mweka Hazina na nafasi tatu za wajumbe wa Kamati ya Utendaji.

"Ada ya fomu kwa nafasi tano za juu ni Sh. 100,000 na kwa nafasi ya ujumbe ni Sh. 50,000. Usaili wa wagombea utafanyika siku mbili kabla ya uchaguzi," alisema ofisa huyo.

Aliongeza, kwa kuwataka wadau wenye sifa kujitokeza kuwania nafasi za uongozi ili chama hicho kipate safu ya viongozi iliyokamilika kwa maendeleo ya mchezo huo.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### NEYMAR KUTUA CHELSEA
CHELSEA imepewa nafasi ya kumsajili, Neymar mwenye umri wa miaka 30, wakati Paris St-Germain wakijaribu kumuuza mshambuliaji huyo wa Brazil ili kuepuka kukiuka miongozo ya Uefa ya usawa wa matumizi ya fedha. ***(Mail)***

### LEAO, ZAKHARYAN SOKONI
MSHAMBULIAJI wa AC Milan, Rafael Leao mwenye umri wa miaka 23 na kiungo wa kati wa Dinamo Moscow, Arsen Zakharyan (19), wamehusishwa na Chelsea. ***(Times)***

### DEST ATUA MILAN
MLINZI wa pembeni wa Barcelona, Sergiño Dest atajiunga na AC Milan kwa mkopo wa msimu mzima, na chaguo la kubadilisha uhamisho huo kuwa wa kudumu wa euro milioni 20. Beki huyo Mmarekani alikuwa akihusishwa kuhamia Manchester United. ***(Fabrizio Romano)***

### MUDRYK ANUKIA BRENTFORD
BRENTFORD ina matumaini ya kuipiku Arsenal na kumnunua Mykhaylo Mudryk mwenye umri wa miaka 21 kutoka Shakhtar Donetsk, lakini itabidi kuvunja rekodi ya uhamisho ya klabu hiyo ili kumsajili mshambuliaji huyo wa Ukraine mwenye thamani ya pauni milioni 25. ***(Mirror)***

### DANILO KUTUA ARSENAL
ARSENAL imefanya mawasiliano na kuwasilisha ofa ya pauni milioni 20 kwa kiungo wa Palmeiras, Danilo mwenye umri wa miaka 21, lakini klabu hiyo inataka ada ya juu zaidi kwa Mbrazil huyo. ***(Goal Brazil via Metro)***

### GAKPO KUONDOKA PSV
PSV Eindhoven imekubali mkataba wa pauni milioni 34 kwa Gakpo huku Southampton ikijiandaa kuvunja rekodi ya uhamisho ya klabu hiyo. ***(Times)***

### ICARDI SAFARI IMEIVA
KLABU ya Fenerbahce imeingia kwenye kinyang'anyiro cha kumnunua fowadi wa Paris St-Germain, Mauro Icardi mwenye umri wa miaka 29, huku mshambuliaji huyo wa Argentina tayari akiwindwa na Galatasaray ya Uturuki. ***(L'Equipe)***

### TIELEMANS NJIA MOJA
KLABU ya Newcastle United imeingia kwenye kinyang'anyiro cha kumsajili kiungo wa kati wa Leicester City na Timu ya Taifa ya Ubelgiji, Youri Tielemans mwenye umri wa miaka 25.***(Mail)***

### ARSENAL YAKATA TAMAA
KLABU ya Arsenal ambayo ilikuwa inamfuatilia Youri Tielemans katika kipindi chote cha dirisha la usajili, lakini "klabu nyingine isiyojulikana" sasa iko tayari kuwasilisha ombi huku Leicester ikiweka bei ya pauni milioni 30. ***(Express)***

### ALVAREZ AITAKA CHELSEA
KIUNGO wa kati wa Ajax, Edson Alvarez mwenye umri wa miaka 24 ana nia ya kutaka kuhamia Chelsea huku mmiliki, Todd Boehly akitoa ofa ya pauni milioni 50 kwa ajili ya kumnunua mchezaji huyo wa kimataifa wa Mexico. ***(De Telegraaf via Metro)***

### BARCA YAWEKA NGUMU
BARCELONA wamekataa ofa ya mchezaji pamoja na fedha kutoka kwa Chelsea kwa mshambuliaji wa Gabon, Pierre-Emerick Aubameyang mwenye umri wa miaka 33. Barca wamesema wanataka euro milioni 15 pamoja na beki wa pembeni wa Hispania, Marcos Alonso (31), lakini mazungumzo yanaendelea. ***(Fabrizio Romano)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# HAALAND HASHIKIKI LIGI KUU ENGLAND

Sasa afikisha mabao tisa na kuiweka City katika nafasi ya pili kwenye...

**MANCHESTER, England**

ERLING Haaland alifunga mabao matatu (hat-trick) kwa mara ya pili mfululizo wakati Manchester City ilipoichapa Nottingham Forest magoli 6-0 katika mechi ya Ligi Kuu England iliyochezwa kwenye Uwanja wa Etihad, Jumatano usiku.

Raia huyo wa Norway alifikisha mabao tisa msimu huu kwenye Ligi Kuu England katika mechi yake ya tano pekee.

Mabayo yote matatu alifunga kipindi cha kwanza huku kikosi kipya cha Steve Cooper kilichopanda daraja kikishindwa kummudu mshambuliaji huyo mpya wa kati wa City.

Bao la ajabu kutoka kwa Joao Cancelo lilifanya yawe manne kabla ya mabao mawili ya Julian Alvarez kwenye mechi yake ya kwanza ya Ligi Kuu England chini ya kikosi hicho cha Pep Guardiola.

Ushindi huo unawafanya mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu England kubakia nafasi ya pili na kupitwa pointi mbili na vinara Arsenal kwenye msimamo, huku Nottingham Forest wakibakia na pointi nne.

City walikuwa katika udhibiti kamili tangu mwanzo wa kipindi cha kwanza na kuwabana kila sehemu Forest.

Bao la kwanza la Haaland lilikuja baada ya kuiwahi krosi ya Phil Foden na la pili likaja muda mfupi baadaye.

Pasi ya mlinda mlango wa Forest, Dean Henderson ilimpata Bernardo Silva ambaye alimsukumia pande Haaland na kufunga la tatu.

Guardiola alifanya mabadiliko mawili katika kikosi chake huku Ilkay Gundogan akiingia kuchukua nafasi ya Kevin De Bruyne na Julian Alvarez akichukua nafasi ya Riyad Mahrez.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,027,3

MECHI KALI
BORUSSIA DORTMUND
VERSUS
HOFFENHEIM
1 | 1.60
X | 4.40
2 | 4.40

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa
vodacom | m-pesa
airtel money
ZANTEL EZYPESA
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# RONALDO SASA KUONDOKA JANUARI




**MANCHESTER, England**

KOCHA Erik ten Hag, amesema Cristiano Ronaldo atabaki Manchester United hadi angalau Januari kama hataki kuendelea kuichezea timu hiyo.

Huku muda wa mwisho wa uhamisho ukifungwa jana, juhudi za Ronaldo kuondoka United kutafuta sehemu ya kwenda kucheza mashindano ya Ligi ya Mabingwa Ulayaziligonga mwamba.

Alipoulizwa kama amezungumza na Ronaldo, bosi wa United, Ten Hag alisema: "Mara kadhaa, ndiyo. Tuko kwenye ukurasa mmoja. (Anafurahia kubaki) vinginevyo hangekuwa hapa."

Kutua kwa mshambuliaji wa Brazil, Antony kutoka Ajax kwa pauni milioni 86 kunaweza kupunguza zaidi muda wa kucheza kwa Ronaldo, ambaye ameanza mechi moja tu ya Ligi Kuu England msimu huu.

"Tangu mwanzo tulisema tulipanga naye (Ronaldo), tunafurahi naye, ana furaha kuwa hapa, na tunataka kufanya msimu uwe wa mafanikio pamoja.

"Halafu pia inahusu maendeleo ya timu, ya mtu binafsi, ili kuifanya timu kuwa na nguvu na thabiti zaidi, ili kuleta ubora zaidi. Hilo ndilo tunalopaswa kulifanyia kazi kwa sasa, mimi pamoja na makocha wangu na umoja na timu."

Kuhusu ni wapi Ronaldo anaingia kwenye falsafa ya soka ya Ten Hag, Mholanzi huyo ameachwa akiwa na uhakika kutokana na uchezaji wa fowadi huyo katika mazoezi ambayo ana jukumu la kutekeleza katika mfumo wowote utakaotumika msimu huu.

# Gerrard ahofia kufukuzwa Villa

**LONDON, England**

STEVEN Gerrard amesema ana wasiwasi kuhusu mustakabali wake kama Kocha wa Aston Villa baada ya timu yake kuchapwa mabao 2-1 na Arsenal kwenye Ligi Kuu England hapo juzi usiku.

Kipigo hicho kilikuwa cha nne kwa Villa katika mechi tano za mwanzo wa msimu huu mpya na kuwaacha wakiwa nafasi ya 19 kwenye msimamo.

Alipoulizwa kama alikuwa na wasiwasi kuhusu kazi yake, Gerrard aliiambia BT Sport: "Bila shaka ninayo.

"Ikiwa ningesimama hapa na kusema sikujali, nadhani ungeniangalia kama ninatoka sayari tofauti."

"Ni ukweli na kujikosoa ni jambo zuri. Nitafanya kazi yangu kadri niwezavyo kufanya," aliongeza Gerrard.

"Nitasonga mbele na kuwajibika kadri niwezavyo. Tulionyesha tabia na kujitolea na tulikuwa tukishikilia wakati fulani, lakini ikiwa tutaendelea kupata wakati muhimu katika maeneo muhimu tutaendelea kuruhusu mabao.

Ushindi pekee wa Villa msimu huu ulikuja nyumbani kwa Everton mapema Agosti, ingawa pia wameshinda Bolton kwenye Kombe la Carabao.



393,141/-

SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 03/09/22 | 17:00 | Swansea City vs Queens Park Rangers | 2.33 | 3.20 | 2.95 |
| 02. 03/09/22 | 17:00 | Rotherham United vs Watford FC | 2.90 | 3.15 | 2.41 |
| 03. 03/09/22 | 19:00 | AC Milan vs Inter Milano | 2.60 | 3.25 | 2.60 |
| 04. 03/09/22 | 19:00 | FC Sion vs FC Basel 1893 | 2.60 | 3.30 | 2.50 |
| 05. 03/09/22 | 19:30 | Real Sociedad San Sebastian vs Atletico Madrid | 2.80 | 3.10 | 2.50 |
| 06. 03/09/22 | 19:30 | SD Ponferradina vs Sporting Gijon | 2.55 | 3.20 | 2.65 |
| 07. 03/09/22 | 20:00 | AC Omonia Nicosia vs AEK Larnaca | 2.50 | 3.35 | 2.60 |
| 08. 03/09/22 | 21:45 | Lazio Rome vs SSC Napoli | 2.80 | 3.35 | 2.36 |
| 09. 04/09/22 | 02:00 | New York Red Bulls vs Philadelphia Union | 2.35 | 3.45 | 2.75 |
| 10. 04/09/22 | 14:00 | Reading FC vs Stoke City | 2.85 | 3.15 | 2.43 |
| 11. 04/09/22 | 14:30 | Hansa Rostock vs Hannover 96 | 2.49 | 3.35 | 2.65 |
| 12. 04/09/22 | 15:00 | Odense Boldklub vs Viborg FF | 2.55 | 3.50 | 2.48 |
| 13. 04/09/22 | 16:00 | AC Ajaccio vs FC Lorient | 2.37 | 3.25 | 2.85 |
| 14. 04/09/22 | 16:00 | Stade Brest 29 vs Strasbourg Alsace | 2.90 | 3.40 | 2.28 |
| 15. 04/09/22 | 17:00 | Huddersfield Town vs Blackpool | 2.55 | 3.15 | 2.70 |
| 16. 04/09/22 | 18:30 | Manchester United vs Arsenal FC | 2.41 | 3.45 | 2.65 |
| 17. 04/09/22 | 21:30 | Aris Thessaloniki vs PAOK Thessaloniki | 2.39 | 3.15 | 2.90 |

MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE
"2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

IJUMAA - 02/09/2022

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 1836 | Daejeon Korail vs Busan Transp. | 2.42 | 3.04 | 2.80 |
| 13:00 | 2143 | B. Binh Duong vs CLB Viettel | 3.29 | 3.24 | 2.05 |
| 13:00 | 5822 | Suwon City vs Jeju Utd | 3.05 | 3.39 | 2.09 |
| 13:30 | 5735 | Consadole Sapporo vs Cerezo Osaka | 2.54 | 3.27 | 2.49 |
| 14:15 | 1472 | Persita Tangerang vs Persepam MU | 2.28 | 3.23 | 2.84 |
| 14:45 | 3281 | Balestier Khalsa vs Albirex Niigata (SIN) | 11.71 | 7.61 | 1.13 |
| 16:00 | 1452 | Van Yerevan vs Ararat Armenia | 7.06 | 3.92 | 1.42 |
| 16:00 | 3107 | Kedah vs Penang | 1.31 | 4.82 | 7.86 |
| 16:00 | 4133 | Alashkert Martuni vs Shirak Gyumri | 1.40 | 4.20 | 6.84 |
| 16:30 | 1315 | CSA Steaua Bucuresti vs FC Politehnica Iasi | 2.23 | 3.09 | 3.05 |
| 17:00 | 4529 | Rukh Vinnyky vs Shakhtar Donetsk | 7.67 | 5.51 | 1.27 |
| 17:30 | 1926 | MSK Zilina vs Sport Podbrezova | 1.84 | 3.52 | 3.67 |
| 17:30 | 5834 | ND Gorica vs NK Mura | 3.84 | 3.64 | 1.77 |
| 18:30 | 2091 | Luka Koper vs NK Celje | 2.26 | 3.20 | 2.91 |
| 18:30 | 5451 | USM Khenchela vs USM Alger | 4.61 | 3.53 | 1.67 |
| 18:45 | 3870 | Sepsi Osk vs CS Mioveni | 1.56 | 3.75 | 5.80 |
| 19:00 | 3305 | Aris Limassol vs Olympiakos Nicosia | 1.93 | 3.43 | 3.84 |
| 19:00 | 3411 | Zaglebie Sosnowiec vs ZKS Stal Rzeszow | 2.19 | 3.29 | 2.95 |
| 19:00 | 3797 | FUS Rabat vs Wydad Casablanca | 3.73 | 2.99 | 2.01 |
| 19:30 | 3899 | Heidenheim vs Fortuna Dusseldorf | 2.43 | 3.26 | 2.76 |
| 20:00 | 2060 | Pafos FC vs Karmiotissa | 1.47 | 4.24 | 6.46 |
| 20:00 | 5076 | Copenhagen vs Silkeborg | 1.71 | 3.93 | 4.23 |
| 20:00 | 5752 | FC Helsingor vs Nykobing FC | 1.26 | 5.32 | 8.46 |
| 20:30 | 1213 | Concarneau vs Nancy | 2.07 | 3.28 | 3.38 |
| 20:30 | 3287 | SuperSport Utd vs Mamelodi Sundowns | 4.59 | 3.34 | 1.78 |
| 21:00 | 2728 | NAC Breda vs FC Eindhoven | 2.22 | 3.39 | 2.94 |
| 21:00 | 3181 | Umraniyespor vs Trabzonspor | 4.43 | 3.83 | 1.70 |
| 21:00 | 3684 | Dinamo Zagreb vs HNK Rijeka | 1.28 | 4.93 | 8.49 |
| 21:00 | 4186 | Benfica vs FC Vizela | 1.19 | 6.64 | 12.08 |
| 21:00 | 4910 | Den Bosch vs PEC Zwolle | 5.18 | 4.39 | 1.51 |
| 21:00 | 5547 | Fortuna Sittard vs Utrecht | 3.46 | 3.56 | 1.96 |
| 21:00 | 5919 | Mezokovesdi SE vs Zalaegerszegi TE | 2.40 | 3.19 | 2.70 |
| 21:15 | 5633 | FC Thun vs Lausanne-Sport | 2.47 | 3.45 | 2.47 |
| 21:30 | 1146 | Universitatea Cluj vs U Craiova SA | 2.67 | 3.02 | 2.67 |
| 21:30 | 1859 | Cagliari vs Modena | 1.83 | 3.45 | 4.10 |
| 21:30 | 4204 | Borussia Dortmund vs Hoffenheim | 1.60 | 4.40 | 4.40 |
| 21:30 | 4407 | Legia Warszawa vs Radomiak Radom | 1.88 | 3.38 | 3.67 |
| 21:45 | 1005 | Bohemians FC vs Shamrock Rovers | 3.48 | 3.24 | 1.98 |
| 21:45 | 1309 | Derry City vs UCD Dublin | 1.16 | 6.12 | 12.83 |
| 21:45 | 1413 | St Patricks vs Finn Harps | 1.48 | 4.02 | 5.69 |
| 21:45 | 2608 | Metz vs Annecy FC | 1.73 | 3.35 | 4.90 |
| 21:45 | 4622 | Brugge vs Cercle Brugge | 1.55 | 4.20 | 5.20 |
| 21:45 | 5268 | Dundalk FC vs Shelbourne | 1.78 | 3.30 | 4.24 |
| 21:45 | 5727 | Cork City vs Longford Town | 1.49 | 4.03 | 5.50 |
| 22:00 | 1403 | MC Oran vs MC Magra | 1.86 | 3.14 | 4.12 |
| 22:00 | 2872 | West Bromwich vs Burnley | 2.23 | 3.20 | 3.15 |
| 22:00 | 4437 | Celta Vigo vs Cadiz CF | 1.69 | 3.57 | 5.03 |
| 22:00 | 4628 | Leganes vs Eibar | 2.55 | 2.96 | 2.86 |
| 23:15 | 3487 | GD Estoril vs Sporting Lisbon | 6.42 | 4.31 | 1.45 |
| 23:30 | 1742 | Ayacucho vs Sport Boys Association | 1.71 | 3.68 | 4.12 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# TWIGA STARS YATAMBA ITATETEA TAJI COSAFA

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Timu ya Soka ya Taifa ya Wanawake (Twiga Stars), Bakari Shime, amesema anaamini kikosi chake kitafanya vizuri katika mashindano ya COSAFA yanayotarajiwa kufanyika kuanzia leo katika mji wa Port Elizabeth nchini Afrika Kusini.

Twiga Stars itaanza kampeni ya kutetea ubingwa wa mashindano hayo leo kwa kuvaana na Comoro.

Akizungumza na gazeti hili kwa njia ya simu jana kutoka Afrika Kusini, Shime alisema Twiga Stars imejiandaa kufanya vizuri katika michuano hiyo kutokana na maandalizi waliyofanya kwa muda mrefu.

Shime alisema kila mchezaji aliyeko katika kikosi hicho amejipanga kuonyesha ubora wake ili kuhakikisha wanafanikia malengo yao.

"Tumefanya maandalizi mazuri na tutaanza kurusha karata ya kwanza kwa kucheza na Comoro kesho (leo), nina imani kubwa tutatwaa ubingwa maana sisi ndio mabingwa watetezi," alisema Shime.

Kocha huyo aliongeza watahakikisha wanashinda michezo yote ya hatua ya makundi ili kupata nafasi ya kutinga hatua ya nusu fainali.

Baada ya mchezo wa leo, Twiga Stars itashuka tena dimbani Septemba 5, mwaka huu kuchuana na Botswana na watamaliza hatua ya makundi Septemba 7, mwaka huu kuwakabili Malawi ambao walicheza nao fainali msimu uliopita.

Kundi A katika mashindano hayo linaundwa na mwenyeji Afrika Kusini, Msumbiji, Angola na Mauritius wakati Lesotho, Zambia, Eswatini na Namibia wanaunda Kundi B huku Kundi C likiwa na Tanzania, Malawi, Comoro na Botswana.




Mkurugenzi wa Masoko wa Kampuni ya GF Truck & Equipment, Salman Karmal (katikati), na Mtendaji Mkuu Geita Gold FC, Simon Shija (kulia) wakibadilisha nyaraka baada kukubali kuidhamini klabu hiyo jijini Dar es Salaam jana. Kushoto ni Meneja Masoko wa kampuni hiyo, Smart Deus. **PICHA: FAUSTINE FELICIANE**

# GF Truck yatua Geita Gold

**Na Faustine Feliciane**

WAWAKILISHI wa Tanzania katika mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika, Geita Gold FC imeingia makubaliano ya udhamini wa mwaka mmoja na Kampuni ya GF Trucks & Equipment.

Udhamini huo utaisaidia Geita Gold FC kufanya vizuri katika michuano hiyo ya kimataifa na Ligi Kuu Tanzania Bara watakayoshiriki.

Meneja Biashara Mkuu wa GF Trucks, Salman Karmali, alisema kampuni hiyo imeamua kuidhamini Geita Gold kutokana na jitihada za klabu hiyo na wanaamini kupitia wao watafikia malengo waliyojiwekea.

"Udhamini wetu unajumuisha fedha ambazo tutatoa kwa klabu lakini kutokana na makubaliano ya pande zote mbili hatuwezi kuainisha kiasi cha pesa, ni udhamini wenye faida kwa pande zote mbili," alisema Karmali.

Naye Ofisa Mtendaji Mkuu wa Geita Gold FC, Simon Shija, alisema kutokana na majukumu waliyonayo msimu huu ujio wa GF Truck utawasaidia kufikia malengo yao.

"Udhamini huu na ushirikiano na wadhamini wengine tulionao kama Anglo Gold Ashanti unatupa uhakika wa kusafiri ndani na nje ya nchi katika mechi za michuano ya CAF," alisema Shija.

# Michezo

Ijumaa Septemba 2, 2022

Nipashe


UKURASA 21



## Haaland hashikiki Ligi Kuu England




Wachezaji wa Timu ya Taifa ya Gofu ya Wanawake inayotarajiwa kushiriki mashindano ya Afrika (All Africa Challenge Trophy 2022), wakionyesha ishara ya ushindi katika michuano itakayofanyika kuanzia Septemba 6, mwaka huu kwenye viwanja vya Gymkhana jijini Dar es Salaam. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# YANGA: KISINDA ATATUBEBA CAF

## •••Winga huyo anatarajiwa kutua nchini mapema ili kuiwahi Azam FC, Wasudan na...

**Shufaa Lyimo na Adam Fungamwango**

WINGA Tuisila Kisinda ambaye amerejea katika kikosi cha Yanga akitokea RS Berkane ya Morocco, anatarajiwa kuwasili nchini muda wowote kwa ajili ya kuungana na nyota wenzake kuelekea mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Azam FC utakaochezwa Septemba 6, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Koçha Msaidizi wa Yanga, Cedrick Kaze, alisema klabu inakamilisha taratibu za safari za mchezaji huyo ambaye alitangazwa kurejea Yanga usiku wa kuamkia jana.

"Kisinda ni mchezaji mzuri na ninaamini ataendeleza ushindani wake kwenye michezo ya Ligi Kuu na mashindano ya kimataifa tunayotarajia kushiriki," alisema Kaze.

Kocha huyo alisema Yanga imesajili wachezaji ambao watawapa mafanikio ndani ya timu hiyo kwa kutetea makombe yote wanayoyashikilia.

Aliongeza wachezaji wao wanaendelea kujiimarisha kuelekea mchezo huo ambao amekiri utakuwa mgumu na wenye ushindani kutokana na wapinzani wao pia kuwa imara.

"Safu yetu ya pembeni ilikuwa na mapungufu, kumpata Kisinda ni faraja kubwa. Ataziba nafasi hiyo ambayo tumebaini na ndio maana tukaamua kumrudisha nyumbani," Kaze alisema.

Mkurugenzi wa Mashindano wa Yanga, Saad Kawemba, alisema wameamua kumrejesha Kisinda ili kukifanya kikosi chao kuwa kipana na chenye wachezaji wengi wenye uwezo unaofanana kwa ajili ya kufanya vyema katika michuano ya kimataifa.

Kawemba alisema usajili wa Mkongomani huyo ni mapendekezo yaliyotolewa na benchi la ufundi la timu yao ambalo liko chini ya Kocha Mkuu, Nasreddine Nabi ambaye anamfahamu vizuri winga huyo.

"Tunatarajia tufanye vizuri, msimu uliopita tulishinda ndani, na tunataka kuendelea tena msimu huu kushinda ligi ya ndani, lakini msimu huu tunafanya jitihada kubwa kuona ni namna gani tunacheza mechi za kimataifa na tunafikia kwenye ngazi ipi, ili tuwe bora kuliko mara ya mwisho tulivyoshiriki. Na hayo ni malengo yetu na benchi la ufundi," alisema Kawemba.

Aliongeza kikubwa walichokusudia ni kuona timu yao ina wachezaji wenye ubora mkubwa wa kushindana na kukabiliana na changamoto mbalimbali.

"Wachezaji ni binadamu na sio mashine, wanachoka, hivyo wachezaji wa akiba wasiwe wanapishana sana kiuwezo na wale walioanza, akitoka huyu akiingia huyu basi mwalimu anapata kile anachokihitaji, na ndicho Wanayanga wachokihitaji," aliongeza bosi huyo.

Kabla ya kuelekea RS Berkane, Yanga ilimsajili Kisinda Agosti, mwaka juzi akitokea AS Vita ya DRC.

Yanga ndio mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara na baada ya kuivaa Azam FC, itashuka tena dimbani kuikaribisha Zalan FC kutoka Sudan Kusini kwenye mchezo wa Ligi ya Mabingwa Afrika.

## Zoran achekelea ubora wa Simba

**Na Saada Akida**

WAKATI kikosi cha Simba kilirejea nchini jana kikitokea Sudan, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Zoran Maki, amefurahishwa na kiwango kilichoonyeshwa na wachezaji wake katika mechi ya kirafiki ya kimataifa ya mwisho waliyocheza dhidi ya wenyeji, Al Hilal hapo juzi.

Maki alisema mechi hiyo imeendelea kuwapa nafasi ya kujiimarisha wachezaji wake na imewasaidia kuwaweka tayari na mapambano katika mechi za Ligi Kuu Bara na mashindano ya kimataifa.

"Ingawa tumefungwa bao 1-0, lakini tumecheza vizuri sana, tulimiliki pia, hatukutengeneza nafasi nyingi katika mechi mbili au tatu zilizopita, kwa mfano nafasi aliyocheza Banda (Peter) ya kiungo ilikuwa bora sana, ilikuwa suprise kubwa kwangu," alisema Maki.

Naye kiungo, Clatous Chama, alisema mechi walizocheza zimewasaidia kuwaimarisha na wanashukuru hawajapata majeraha kwenye michuano hiyo maalumu waliyoshiriki.

"Kuna baadhi ya wachezaji walikosekana, lakini hii ni timu na kila mmoja alijaribu kuonyesha uwezo wake, tumepata nafasi ya kujijenga, imetupa nafasi ya kujifunza sisi na benchi la ufundi tukiwa kwenye maandalizi ya kuelekea Malawi," Chama alisema.

Wakati huo huo, Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, alisema uongozi wa klabu hiyo umeweka wazi beki wao, Joash Onyango, hataondoka katika kikosi hicho na badala yake atatakiwa kupambana kupata namba.

"Bado ana mkataba ambao unamfunga, ataendelea kuwapo kikosini na yupo katika mipango ya benchi lao la ufundi," Ahmed alisema.

Alisema baada ya kurejea nchini jana wataingia kambini kwa ajili ya kujiandaa na mchezo mwingine wa kirafiki wa kimataifa dhidi ya Arta Solar 7 kutoka Djibouti ili kujiimarisha kuelekea mechi yao ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya KMC FC itakayochezwa Septemba 7, mwaka huu.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >